

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NANE**

Kikao cha Tisa – Tarehe 15 Septemba, 2017

(Bunge Lilanza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tuli'a Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2015/2016 (*The Annual Report and Accounts of the Local Authority Pensions Fund (LAPF) for the Year 2015/2016*).

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Mfuko wa Fedha za Barabara kwa mwaka 2013/2014 (*The Annual Report and Accounts of Fund Board for the Year 2013/2014*).

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na.105

**Ujenzi wa Daraja – Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAY** aliuliza:-

Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilipeleka maombi maalum ya fedha za ujenzi wa daraja la Gunyoda na wakati huo kutokana na kugawanywa kwa Wilaya ya Mbulu kupata Wilaya mbili, daraja la Gunyoda limebaki kuwa kiungo muhimu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na Halmashauri ya Mbulu vijijini.

Serikali Kuu ilitoa kiasi cha Sh.100,000,000/= ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Mbulu kwa maagizo ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne fedha hizo zilelekezwa kwenye ujenzi wa maabara za sayansi katika Halmashauri zote nchini na kuacha daraja hilo bila kujengwa kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu haina uwezo wa kulijenga kwa fedha za ndani:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi wa daraja hilo ambalo ni kikwazo kikubwa kwa huduma za kijamii katika Halmashauri zote mbili?

(b) Kwa kuwa mabadiliko ya Tabianchi yamesababisha uwepo wa makorongo makubwa ambayo yako katika Kata za Gonyoda, Silaloda, Gedamara, Bargish, Dandi, Marangw' na Ayamaami jambo linalosababisha jamii kukosa huduma za jamii, afya na utawala. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta fedha za dharura ili kusaidia janga hilo katika Halmashauri mbalimbali ikiwemo Mbulu Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Mbulu linalopita kwenye Korongo la Gunyoda lenye urefu wa mita 70.4 na kina cha mita tano lilifanyiwa usanifu wa awali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na kubaini kwamba zinahitajika shilingi milioni mia nane na hamsini kulijenga. Hadi sasa ni muda mrefu umepita, hivyo Serikali kupitia Wataalam wa Halmashauri itafanya usanifu wa kina kujua gharama halisi za kuingiza katika mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019 ili kuanza ujenzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwcaa wa fedha 2017/2018 Serikali inaanza utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambaa utatekelezwa kwenye halmashauri 15 ili kuandaa mpango wa kuzingatia athari za tabianchi. Serikali itashirikiana kikamilifu na halmashauri ili kuhakikisha fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya matengenezo ya dharura. Natoa wito kwetu sote kwa pamoja tushirikiane kikamilifu katika kutunza mazingira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wetu, hali hii ya makorongo na jiografia inayobadilika kutokana na tabianchi imesababisha jamii yetu hasa akinamama kukosa huduma za afya, watoto na wanafunzi kukosa masomo na kwa kuwa ni tatizo la nchi nzima, je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuona ni namna gani hata madaraja ya dharura kama yale ya chuma kuwekwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, sasa hivi tunabadilika kutoka Watendaji wa Halmashauri na barabara zote zinazohudumiwa na Halmashauri zinapelekwa kwa Wakala wa Barabara za Vijijini. Je, ni kwa namna gani Serikali itatazama suala hili kutokana na kwamba fedha zinazotengwa ni kidogo sana kulingana na fedha za Mfuko wa Barabara kwa zile barabara zilizokuwa zinahudumiwa na halmashauri za wilaya katika maeneo ya vijijini ili fedha zitakazotengwa kwa dharura ziweze kusaidia tatizo hili na jamii ipate huduma stahiki na kwa wakati kuliko sasa ambavyo inapoteza maisha katika hali ya dharura na mvua nyakati za masika? Ahsante. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika nchi yetu kuna maeneo mbalimbali yanaathirika sana, na hasa katika Mkoa ule wa Manyara. Nikiri wazi kwamba eneo lile lina changamoto kubwa sana na wakati mwingine mvua ikinyesha utakuta sehemu nyingine mpaka mito inahama. Hali hiyo inajitokeza hata katika Mkoa huu wetu wa Dodoma na Mkoa wa Morogoro maeneo ya Gairo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa suala la upatikanaji wa madaraja ya chuma naomba tu niseme kwamba jambo hilo tumelipokea, japokuwa siwezi kusema kwamba hilo daraja litapatikana lini; lakini kwa haja ya kusaidia wananchi nadhani ngoja tuliweke hilo katika vipaumbele vyetu. Katika maeneo ambayo mwanzo yalikuwepo madaraja hayo, lakini leo hii yametengenezwa madaraja mengine, yale madaraja ambayo ni ya chuma yaliyohamishwa kule, tutaangalia jinsi ya kufanya, kwa kushirkiana na wenzetu wa TANROADS katika maeneo mbalimbali ili kusaidia jamii yetu hasa kule Mbulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la TARURA na bajeti; ni kweli katika fedha zinazokwenda za Mfuko wa Barabara; kwa sababu kuna ule mgawanyo wa sheria ambapo sheria ya TANROADS ni tofauti na sheria za halmashauri; lakini tumeunda Wakala mpya ambao una mikakati vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine linalofanyika ni suala zima la resource mobilization, kutafuta fedha, kwa hiyo naamini; katika kipindi hiki ambacho TARURA inaanza sasa naomba Waheshimiwa Wabunge muwe na imani, kwamba kazi nzuri itafanyika na mtakuja kuona kwamba kuna faida kubwa sana kwa kuanzisha Wakala huu; ambapo ilianishwa wazi katika ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwamba lazima katika kipindi hiki Wakala uanzishwe. Sisi jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tutasimamia Wakala huu ili uweze kufanya kazi vizuri ili wananchi waweze kupata huduma vizuri

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijaendelea niwakumbushe tu; maswali tuulize kwa kifupi ili tupate majibu mahususi. Ukishauliza na maneno mengi na wewe unajibowi kwa maneno mengi; kwa hiyo pande zote mbili maneno kwa kifupi tafadhali.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.106

#### **Mfuko wa Maendeleo ya Jamii**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Mwaka 2000 Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ili kusaidiana na vyombo vingine vyta Serikali kupunguza umaskini:-

Je, hali ya utekelezaji wa mpango huo wa TASAF ikoje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mwaka 2000 ili kusaidiana na vyombo vingine vya Serikali kupunguza umaskini. Mafanikio makubwa yamepatikana katika awamu zote za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa awamu ya kwanza ambayo ilitekelezwa mwaka 2000 hadi mwaka 2005 iliwezesha jamii kutekeleza miradi 1,704 yenye thamani ya shilingi bilioni sabini na mbili katika halmashauri 40 za Tanzania bara na wilaya zote za Tanzania Zanzibar. Miradi hiyo iliibuliwa na wananchi na ilihuisha sekta zote muhimu za afya, elimu, maji pamoja na barabara vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa awamu ya pili, TASAF ilitekelezwa mwaka 2005 hadi mwezi Juni, 2013 ambapo miradi 12,347 yenye thamani ya shilingi bilioni 430 katika halmashauri 126 za Tanzania Bara na wilaya zote za Tanzania Zanzibar. Miradi hii iliongeza upatikanaji wa huduma za maji, elimu, afya, pamoja na barabara vijijini na kuongeza upatikanaji wa chakula

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya tatu ilizinduliwa mwaka 2012 na utekelezaji wake uliana mwezi Januari, 2013 na unaendelea kutekelezwa hadi mwaka 2022 katika halmashauri 159 za Tanzania Bara na wilaya zote za Tanzania Zanzibar. Madhumuni ya TASAF awamu ya tatu ni kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato, fursa pamoja na uwezo wa kuwagharamia mahitaji muhimu. Kazi zilizofanyika katika awamu ya tatu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kaya maskini milioni 1.1 zenye jumla ya watu takribani milioni tano zimeandikishwa katika vijiji, mitaa na shehia 9,986. Hadi kufikia mwezi Agosti mwaka huu kaya hizi masikini zilishapokea ruzuku ya shilingi bilioni 521.9. Kaya hizo pia zimetekeliza miradi ya kutoa ajira za muda kwa kaya za walengwa 354,648 kutoka katika halmashauri 42 za Tanzania Bara pamoja na Tanzania Zanzibar. Hadi kufikia Agosti mwaka huu, jumla ya miradi 3,553 yenye thamani ya shilingi bilioni 51.1 kutoka katika vijiji 2,063, mitaa 329 na shehia 168 imeibuliwa na kutekelezwa. Hadi sasa miradi 2,952 imekamilika; lakini pia miradi 601 iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa kukamilishwa katika mwaka huu wa fedha

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Agosti mwaka huu, miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii 192 yenye thamani ya shilingi bilioni nane imetekeliza Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, mpango wa kuhamasisha kaya kuweka akiba na kuwekeza unatekelezwa na umewawezesha walengwa kushiriki katika kuweka akiba katika vikundi na kutekeleza miradi ya ujasiriamali ikiwa ni mkakati endelevu wa kaya kutoka kwenye umaskini. Jumla ya vikundi 5,136 vya kuweka akiba na kuwekeza vyenye wanachama 11,907 vimeundwa katika Halmashauri sita za Tanzania Bara ambazo ni Kibaha, Bagamoyo, Chamwino, Lindi, Mtwara pamoja na Manispaa ya Lindi, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukurru sana. Naomba tu nimuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nianze na kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kuhakikisha kwamba kaya maskini angalau zinaweza kunufaika na huu mpango wa TASAF na kwa kweli katika mkoa wetu kaya nyingi zimeweza kunufaika na mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Manispaa yetu ya Iringa ambayo ipo Jimbo la Iringa Mjini tuna mitaa 192 na mitaa 98 tu ndiyo ambayo imeweza kunufaika na mpango huu na kuna mitaa 84 ambayo bado haijaweza kufikiwa kabisa na mpango huu wa TASAF; kwa

mfano kwenye Kata ya Nduli kuna mitaa ya Kisoeyo, Mikoba, Kilimahewa, Mgongo na Njiapanda na kwenye Kata ya Kituli kuna mtaa wa Hoho; Kata ya Mkwawa kuna mtaa wa Mosi. Je, ni lini Serikali sasa itazifika kaya hizi maana hali ya kaya katika mitaa hii ni mbaya kuliko hata zile ambazo zimeweza kufikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nina swalii linge la pili. Kwa kuwa zipo kaya ambazo ni maskini na pia zina watoto wenyewe ulemavu. Kwa mfano katika Mkao wetu wa Iringa kwenye Jimbo la Kilolo, Kijiji cha Lulanzi, kuna kaya ambayo ina watoto wanenye, wote wana ulemavu na baba yao amepooza, mama yao sasa hivi amevunjika mguu. Je, katika mpango huu Serikali inawasaidiaje watu ambao tayari ni maskini na hawawezi kufanya kitu chochote katika kuwasaidia ili waweze kupata miradi? Kwa mfano labda kujengewa/kuwekewa mradi wa kisima ambao wanaweza wakauza maji wakiwa pale pale au wakapewa bajaji ili kuweza kunusuru kaya ambazo ni walemvu halafu ni maskini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA**

**BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa niseme Serikali inakubali kwamba ni kweli si vijiji vyote, mitaa, kata na shehia nchini mwetu zimeweza kufikiwa na mpango huu wa TASAF. Ni takriban asilimia 70 tu kama nilivyoeleza ya vijiji, kata, shehia 9,989 ndiyo imefikiwa. Napenda tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa tumeanza taratibu, tunasubiri tu fedha zitakapotoka tuweze kuendelea na zoezi la kuwatambua na kuwaandikisha walengwa liweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia sasa hivi tuko katika mpango tuliokuwa tunamalizia kipindi cha kwanza cha awamu ya tatu ya TASAF ambayo itamalizika mwaka 2018 kuelekea 2019; na sasa hivi tumeanza kusanifu awamu nyingine na tunaamini pia katika zoezi hilo nalo pia tutaendelea kufanya utambuzi na kujuu program itakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pindi tu fedha zitakopatikana tutaweza kuendelea na zoezi la utambuzi wa walengwa na kuweza kuwaandikisha. Vile vile tutakapoendelea katika kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF tunaamini walengwa wataweza kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili amezungumzia kaya za watu ambao ni maskini ambao unakuta ni watu wenyewe ulemavu. Nipende tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati program hii ya TASAF awamu ya tatu inasanifiwa, suala zima la ulemavu halikuwa kigezo, kigezo kilikuwa ni umaskini lakini pia walikuwa wanaangalia umaskini wa kaya nzima kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika aina za ruzuku ambazo zinatolewa, ruzuku ya kwanza kabisa ambayo inatolewa bila hata masharti ya kuangalia kama familia ina watoto ilikuwa inatolewa kwa kaya nzima. Hata hivyo, nipende kusema, endapo kaya hiyo ina watu wenyewe ulemavu ambao wako chini ya miaka minane walikuwa wanakuwa treated au wanahesabiwa kama watoto wengine katika familia hiyo kwa mujibu wa ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa familia ambazo tumezikuta zina ulemavu wamekuwa wakishirikishwa katika miradi mbalimbali ya ajira ya muda. Hata hivyo, bado kama alivyoyeleza yeye tulipata changamoto, ziko familia ambazo unakuta zina watu ambao wamezidi miaka 18, hata wakipewa ajira ya muda wengine ni mpaka wabebwe na hawawezi kufikia katika hiyo miradi mbalimbali. Niseme tu, tumelipokea na sasa hivi tunaposanifu awamu ya tatu ya mradi

huu tutaendelea kuliangalia; kwamba katika awamu nyingine ni nini kifanyike kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu lakini pia kwa sasa tunaangalia tunaweza tukawasaidiaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Ndassa, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. TASAF awamu ya pili ilianzisha mradi wa barabara ya Bungurwa-Msunga; leo ni zaidi ya miaka 10 na yapo makalvati yapo tayari zaidi ya 50. Je, ni lini sasa mradi huo au ujenzi wa barabara hiyo utatekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kama nitakuwa nimemsikia vizuri; ni kwamba kuna mradi wa makalvati ambao ulikuwa haujamalizika na anataka kufahamu ni lini labda utatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kusema kwamba, tulipotekeleza TASAF awamu ya kwanza na awamu ya pili ni kweli iko miradi ambayo haikuweza kukamilika. Hata hivyo kwa maelekezo ambayo Serikali iliyatoa; tulitoa maelekezo kwa halmashauri zetu kuhakikisha kwamba wanaorodhesha miradi yote ambayo walikuwa hawajatekeleza au imeanza kutekelezwa lakini haijakamilika waweze kutengea fedha katika bajeti ili iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tutafuutilia mradi huo wa kalvati katika Kata ya Misungwi ili tuone ni hatua gani imefikiwa ili mradi huo uweze kukamilika mapema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nuru Bafadhili, swali la nyongeza.

**MHE. NURU AWADH BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna baadhi ya kaya ambazo ni maskini sana lakini hazikuorodheshwa katika zoezi hili la kuwezeshwa katika mradi huu wa TASAF na kuna wengine wana uwezo lakini vile vile wanapokea pesa hizi za TASAF; je, Serikali inatuambia nini kuhusu hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nipende kusema kwamba ni kweli ziko kaya ambazo zilikuwa ni kaya maskini sana lakini unakuta haijaorodheshwa katika mpango na kinyume chake kaya ambazo si maskini au angalau zina ahueni ziliorodheshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika mchakato huu mzima wa uandikishwaji wa walengwa, ni mikutano yetu mikuu katika kata, kijiji na shehia ambayo inashirikishwa. Kwa kiasi kikubwa baadhi yao katika mikutano mingine mikuu unakuta itikadi za kisiasa zimetumika lakini pia unakuta kuna wengine wameorodheshwa wanaogopa kusema kuwabaini kwamba huyu ameingizwa lakini hastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kutoa rai kwa wananchi wetu pamoja na mikutano mikuu, watakapoona kuna kaya zimeorodheshwa hazistahili basi waweze kutoa ushirikiano na waweze kuziondoa na tunaamini wataweza kufanya hivyo kwa sababu mpaka sasa

tumeshaoondoa zaidi ya kaya 73,851 na tutaendelea kufanya hivyo. Tunaomba wananchi waweze kutoa ushirikiano ili wawe ni wale tu ambao kweli wanazo sifa ndio waweze kunufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 107

**Adaptation Fund**

**MHE. UPENDO F. PENEZA** aliuliza:-

Je, Serikali inatumiaje fedha za Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabia Nchi (Adaptation Fund) zinazotolewa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabia nchi (Adaptation Fund AF) chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi zilizotolewa mwaka 2013 zinatumika kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Jiji la Dar-es-Salaam. Gharama za mradi huu ni Dola za Marekani milioni tano na zinatekeleza kama ifuatavyo:-

(i) Kujenga ukuta wa bahari katika maeneo ya Barabara ya Obama (zamani Ocean Road wenyewe urefu wa mita 820) na Kigamboni (Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere wenyewe urefu wa mita 380)

(ii) Kujenga miundombinu ya mitaro ya maji ya mvua katika Mtaa wa Bungoni, Kata ya Buguruni, wenyewe urefu wa mita 1,003 na Mtaa wa Miburani, Kata ya Mtoni wenyewe urefu wa mita 800.

(iii) Kurudisha matumbawe katika ukanda wa Bahari ya Hindi, eneo la Sinda, Dar-es-Salaam lenye ukubwa wa mita za mraba 2000.

(iv) Kuendesha mafunzo kuhusu matumizi endelevu ya nishati na kusambaza majiko banifu kwa familia 3000 za Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni.

(v) Kupanda mikoko katika eneo la takribani hekari 40 katika maeneo ya fukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund) hutolewa kuititia njia mbili, yaani Mawakala wa Kimataifa (Multination Implementing Entities – MIEs) na Taasisi za Kitaifa (National Entities – NIEs) ambazo zimesajiliwa (accredited) na mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi unaotekelezwa katika Mkoa wa Dar-es-Salaam fedha zake zote zimetolewa kupitia katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Hifadhi ya Mazingira (UNEP) ambaye ni Wakala wa Kimataifa. Ili kuweza kupata fedha nyingine Serikali inakamilisha sasa mchakato ambapo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) inatarajia kusajiliwa (accredited) baada ya kukamilisha masharti yanayohitajika kuwa Taasisi ya Kitaifa ya kuratibu fedha zinazotolewa na Mfuko huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Upendo Peneza, swalii la nyongeza.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuangalia mpango wa kitaifa ambao ulikuwa umeweka vipaumbele 13 ambao ni *National Adaptation Program of Action* kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi Serikali iliweka vipaumbele 13 ambavyo vyta kwanza vilihusu masuala ya maji pamoja na kilimo, lakini katika utekelezaji Serikali hela iliyopata imeweka katika ujengaji wa ukuta katika barabara ya Ocean Road na miundombinu mingine katika maeneo ya Dar-es-Salaam. Sasa Serikali haioni kwamba, inaruka vipaumbele vyake ambavyo iliviweka mwanzo na inakwamisha sasa kuhakikisha kwamba, nchi inakuwa na uwezo wa kuwa na uhakika wa suala zima la usalama wa chakula katika kuangalia hilo suala la vipaumbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ni katika suala zima la NEMC ambalo lilichaguliwa na Makamu wa Rais, ili kuweza kupata hii ithibati. Imechukua sasa miaka mitano kupata hii accreditation na NEMC hawajaweza kupata. Tunavyopata pesa kupitia *Multinational Implementation Entities* Serikali inakatwa asilimia 10 na hizo taasisi kwa hiyo, NEMC iliyopata hizo hela tulikatwa asilimia 10 kwa hiyo, inapunguza hela ambazo zingesaidia katika utekelezaji wa miradi ya kuweza kupunguza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali ina mkakati gani na lini hasa kwa sababu, NEMC imeshachukua miaka mitano, Serikali sasa ni lini itakamilisha mchakato mzima na kukamilisha vigezo vyote, ili hatimaye Serikali iweze kuwa inapata hela zake moja kwa moja? (Makofisi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa niaba ya Waziri wa Muungano na Mazingira.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, linahusu Serikali ilikuwa imeweka vipaumbele 13, lakini Serikali ikaamua kuchukua mradi ule wa Dar-es-Salaam kuhakikisha kwamba, wanaokoa fukwe zetu na kutekeleza shughuli zile ambazo zinahusu kutengeneza mifereji ya maji ya mvua na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, vipaumbele vyote ni muhimu, lakini pia tunaangalia katika vipaumbele vile, ukiacha pembeni kipaumbele ambacho tumeshaanza kukifanya kazi, huwezi ukasema kwamba, hakina umuhimu kuliko hiyo ya kilimo. Hata hivyo, niseme tu kwamba, kama anavyojua katika ombi mradi huu una sehemu ya pili ambayo sasa hivi Serikali inaifanya kazi. Suala la kusema kwamba labda NEMC imechukua muda mrefu, sasa miaka mitano kufanya process ya kupata usajili, ili iweze yenyewe moja kwa moja kuomba sehemu ya pili ya fedha hizi, kwa sababu najua kwamba ilikuwa inatakiwa iwe milioni kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Peneza kwamba tayari NEMC imeshapita vile vigezo vyote ambavyo vilikuwa vimewekwa na hivi karibuni itaanza sasa yenyewe. Itapata usajili na kuanza kuomba ile sehemu ya pili ya fedha ambazo zinatakiwa kuokoa mazingira yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimwambie tu kwamba, NEMC baada ya kupata huu usajili itaanza sasa kuangalia hivi vipaumbele ambavyo yeye amevizungumzia; kuhusu mambo

ya kilimo. Vile vile labda nimwambie kwamba licha ya Serikali kutumia Mfuko huu wa Adaptation Fund tuna Mifuko mingine ambayo pia inaangalia masuala ya kilimo na umwagiliaji. Kwa hiyo, labda nimhakikishie tu kwamba, baada ya NEMC kupewa usajili ambaa tayari imeshapita katika vigezo vile, sasa hivi tunasubiri wapewe hiyo barua ya accreditation ili waweze kuianza hii process ya kuchukua hizi hela milioni tano.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Ally Ungando, sasa aulize swali lake; Mheshimiwa Hawa Mchafu kwa niaba.

Na. 108

### **Mamlaka ya Mji - Kibiti**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA (K.n.y. MHE. ALLY S. UNGANDO)** aliuliza:-

Wananchi wa Mji wa Kibiti wamefanikiwa kupata mradi wa maji, ingawa una changamoto nyingi katika utendaji wake:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku kwa ajili ya kulipia umeme na kulipa vibarua?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza usambazaji maji na mtandao, hasa ikizingatiwa kuwa, Mji huo unaendelea kukua kwa kasi?

### **WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimia Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti, lenye Sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu juu ya gharama zinazohusika katika uendeshaji wa Mamlaka za Maji kuwa ni pamoja na kulipa umeme na wafanyakazi wanaohusika katika uendeshaji huo. Kwa mujibu wa Sheria Namba 12 ya Huduma ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009, Halmashauri za Wilaya zimepewa wajibu wa kusimamia uendeshaji wa mamlaka katika kutoa huduma ya maji safi kwa wananchi katika miji yao, hivyo ni matarajio ya Serikali kuwa, Halmashauri ya Mji wa Kibiti inatimiza wajibu wake huo kwa kuwezesha ugharamiaji kwa kupertia bajeti zake na makusanyo kutohana na matumizi ya maji katika Mji wa Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafahamu ongezeko kubwa la watu linalosababisha kupanuka pia kwa eneo la Mji wa Kibiti. Kwa ufahamu huo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, jumla ya Sh.568,477,000/= zimetengwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya mji safi na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Mji wa Kibiti. Fedha hizo zitatumika katika kuongeza mtandao wa mabomba wenye umbali wa kilometra tano pamoja na kufufua visima vilivyopo ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Kibiti, itaendelea na uvezeshaji katika ujenzi wa miradi ya maji kwa lengo la kuongeza na kuboresha zaidi upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Mji wa Kibiti na Tanzania kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, visima vilivyopo Kibiti vinazalisha maji kidogo tu, lita 4,000; na kwa kuwa, mahitaji ya maji kwa sasa kwa wananchi wa Kibiti ni zaidi ya lita 8,000 hivi ni kwa nini Serikali isianzishe mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Rufiji ili uwafae wananchi wa Rufiji, Kibiti, Kisarawe, Mkuranga na Dar-es-Salaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, kuungua-ungua kwa mota mara kwa mara husababishwa na kukatika kwa umeme mara kwa mara. Nini sasa mpango wa Serikali katika kumaliza kadhia hiyo ili wananchi wa Kibiti waweze kunufaika na mradi huo wa Kibiti? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli anavyosema kwamba uzalishaji ni mdogo kuliko mahitaji na hili ni jambo ambalo liko maeneo mengi; lakini tunayashughulikia yote haya kwa awamu kulingana na bajeti inayotengwa na Serikali. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuangalia namna ya kuongeza uwezo wa uzalishaji wa maji, ili kukidhi mahitaji yaliyopo. Hata hivyo, tumeipangia kwamba, kwa sasa hivi uzalishaji wa pale unakidhi asilimia 70 ya wananchi wa Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali tunataka ikifika mwaka 2020 tufikishe asilimia 85 kwa hiyo, tutaongeza vyanzo vingine ili kusudi tuweze kufikisha lengo ambalo tumelipanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la kuungua-ungua kwa mota. Hili ni tatizo la mahitaji na uendeshaji ni lazima vitu kama hivyo vinaweza vikatokea. Kuungua kwa mota inawezekana pengine ni matatizo ya umeme unapo-flactuate kuwa mkubwa sana kuliko capacity ya zile mota, zitaungua. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Nishati kurekebisha ule umeme unaopatikana pale uwe angalau hauleti madhara ya kuunguaungua kwa mota ambazo zimebekwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Serikali imejenga mradi wa maji katika Mji Mdogo wa Laela ulioanza mwaka 2014 na umetumia takribani shilingi bilioni moja na milioni mia nne; na mradi huu unaonekana umekwisha, lakini cha ajabu hautoi maji, jambo ambalo limeleta tataruki kubwa sana kwa wananchi wa Mji Mdogo wa Laela. Je, ni lini Serikali itahakikisha maji yanatoka katika mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu Mradi wa Mji wa Laela ambaeo Mheshimiwa anauzungumzia nimeutembelea na nimeona umefikia hatua za mwisho, walikuwa katika ufungaji wa zile solar panels. Sasa katika ufungaji wa solar panels kukatokea kwamba ile mota ambayo iliwekwa haiendani na ukubwa wa zile panels. Kwa hiyo nimetuma wataalam waende kule wakaangalie namna ya kutatua tatizo hilo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha mradi ule ambaeo umetumia fedha nydingi za Serikali unafanya kazi kwa manufaa ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Kunakuwa na matatizo mengi ya miradi mingi ya maji nchini ambayo haikamiliki kutopteka na matatizo ya fedha, lakini mara nydingi tukiuliza hapa, nakumbuka Bunge

lilopita, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii alikuwa anasema kwamba Wakurugenzi wetu wakamilishe taratibu za manunuizi, pesa zipo kwenye Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokwenda kwenye halmashauri yangu kwa mfano, nilienda kuulizia suala hili wakasema wameshaandika maandiko mengi kupeleka Wizarani, lakini mpaka leo hawaajaletewa hizo pesa na miradi mingi imekwama . Sasa naomba kupata Kauli ya Serikali; ni nini Kauli ya Serikali kwa miradi ile ya maji iliyokwama kwenye halmashauri zetu mbalimbali hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza; kulingana na fedha za utekelezaji wa miradi zinazopelekwa kwenye halmashauri; tumetoa mwongozo kwamba katika bajeti ambayo kila halmashauri imetengewa wanaweka vipaumbele, wakishaleta andiko Wizarani sisi tunaidhinisha wafanye manunuizi. Wakishafanya manunuizi wakaajiri mkandarasi au mhandisi mshauri tunapeleka fedha kulingana na certificate. Maeneo mengi, halmashauri nydingi zimefuata mwongozo huu na miradi inbaendelea kutekelezwa. Sasa namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya Bunge hili tukutane tuweze kuona, labda kuna tatizo mahususi katika halmashauri ya wilaya yake.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza, Mheshimiwa Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, nilishamwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, wataalam wa utafiti wa visima vya maji, visima ambavyo vitatoa maji baridi wafike na kufanya utafiti wa visima hivyo. Kwa sasa wananchi wa Mji wa Mpwapwa wanatumia maji ya chumvi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu ombi langu hilo la kutafiti visima vingine vya maji baridi, ni lini atalitekeleza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lubeleje, kumbe ulishapeleka maombi. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, ameomba kupata watafiti wa kuweza kugundua maji yaliyoko chini ya ardhi kama yana chumvi au hayana chumvi. Utaalam wa namna hiyo, kwanza haupo. Ni kwamba, lazima kwanza tuchimbe, tuyapate yale maji tukayapime ndipo tutajua yana chumvi na chumvi kiasi gani na kama inahimilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tutakachofanya ni kwamba, tunakwenda kufanya tu tafiti kuona kwamba maji yapo mahali fulani, yatachimbwa halafu tutayapima na kuweza kuona. Kwa hiyo, wataalam hawa tutawapeleka kama anavyoomba, lakini kwa maana ya kujua maji yaliyopo pale, ni lazima kwanza tuyachimbe ndiyo tuweze kujua kama yana chumvi au hayana chumvi.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda, Mbunge wa Malinyi, sasa aulize swali lake.

### **Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji – Itete**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA** aliuliza:-

Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (SAGCOT) imekamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji, Itete ambapo imehusisha ujenzi wa miundombinu ya banio na mfereji mkuu wa kilometa 6.6, lakini katika kipindi kifupi cha matumizi ya skimu hii mfereji huo mkubwa umeshaanza kuharibika kutokana na kiwango duni cha ujenzi:-

(a) Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa mfereji mkuu na mifereji ya kat, ili kuendeleza kilimo katika hekta 7,000 zilizobaki katika skimu hiyo?

(b) Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa mfereji mkuu uliobomoka katika kipindi hiki cha uangalizi?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mbunge wa Jimbo la Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi wa umwagiliaji katika Skimu ya Itete ulianza mwezi Mei, 2013 na kukamilika mwezi Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, upanuzi wa mradi huu unategemea kwa kiwango kikubwa kiasi cha maji katika Mto Mchilipa, kwani usanifu wa awali ulibainisha hekta 1,000 ambazo ndizo zilizoendelezwa. Ili kuweza kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika eneo liliobaki Serikali inajipanga kufanya upembuza yakinifu kuona kama kuna uwezekano wa kujenga bwawa ili kutunza maji ya mvua ya Mto Mchilipa, ambayo yatatumika katika kuendeleza eneo liliobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ndogo iliyobomoka ya mfereji, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Kanda ya Morogoro imeshafanya mawasiliano na Mkandarasi aliyejenga skimu hiyo na amekubali kufanya marekebisho katika sehemu hiyo katika kipindi cha uangalizi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mponda, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Nabu Spika, usimamizi na ushauri wa kitaalam wa jinsi ya uendeshaji wa Skimu hii ya Itete unafanywa na wataalam ambao wanakaa Makao Makuu Malinyi, kilometa 80 kutoka ilipo skimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umbali huo na uhaba mkubwa unaoikabili Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi watumishi hao, wataalam hao wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya kikazi. Je, Serikali hasa Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji mnaisaidiaje Halmashauri ya Malinyi, ili kuwezesha skimu hii ifanye kazi kwa kiwango chake hata kuwapatia gari lilitumika tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, eneo hili la Malinyi lina neema kubwa ya mito ambayo inatiririka maji masika na kiangazi ambayo kama ikitumika vyema tutaweza kumaliza kabisa tatizo la uhaba wa chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu fupi sana; Serikali ina mpango gani sasa kuweza kuongeza skimu nyingine katika Wilaya ya Malinyi kwenye mito kama ya Sofi, Laswesa, Mwatisi, Fuluwa pamoja na Mto wa Mafinji ambayo kama itawekewa skimu tatizo la uhaba wa chakula hasa mpunga, litakuwa limeondoka kabisa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza anazungumzia habari ya usimamizi wa scheme ambayo tayari imeendelezwa na Tume yetu ya Taifa ya Umwagiliaji. Katika mwaka huu wa fedha tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya mapitio ya kuangalia hizi scheme zote ambazo zimejengwa kwa miaka mingi na kuweza kupanga namna bora ya kuziendeleza ikiwa ni pamoja na kuzisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunajipanga katika mwaka wa fedha huu unaokuja tuweze kuangalia scheme zile kubwa ambazo kwanza kulingana na sera tulikuwa tunakabidhi kwa Halmashauri au jumuiya ya watumiaji kuziendesha, lakini maeneo mengi tumeona kwamba hayaendi na jinsi tunavyopanga. Kwa hiyo, tunafanya mapitio na kuona namna bora ya kuweza kuweza kuziangalia namna ya kuzisimamia scheme hizi kwa ajili ya faida ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; ni kweli Wilaya yake ina mito mingi na ndio maana tumesema Tume ya Taifa inafanya kazi ya mapitio ya mpango kabambe wa sera yetu ya Umwagiliaji na kuona namna gani bora tunaweza kuyaendeleza maeneo haya kwa kuweza hata kuwakaribisha wawekezaji wakubwa ili wajenge miradi mikubwa ya umwagiliaji katika maeneo ambayo maji yanaweza kupatikana kwa urahisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku nimekuwa nikilalamika hapa kwamba Wilaya ya Songwe, Mkao mpya wa Songwe na hasa Jimbo langu lina Vijiji sita tu vyenye kutoa maji, vijiji vingine vyote 28 hakuna maji. Je, ni lini yeye mwenyewe kama Waziri anakuja Songwe mimi na yeye tutembee siku nzima nimwoneshe sehemu ambazo wananchi wa Songwe wanalamika maji, hususan ni maeneo ya Mbangala, Mbotoe na Mkajuni. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini nitatembelea Wilaya ya Songwe, nimepanga kuanzia Jumatatu kufanya ziara katika Mikoa ya Ruvuma na Songwe. Kwa hiyo, nitakwenda Songwe kwenda kuangalia malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge na tuweze kuona namna ya kusaidiana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kama ulisema na Mbeya unaenda hivi, umeshaahirisha, naona umetaja mikoa miwili tu hapa. (Kicheko)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara hiyo nitakwenda Ruvuma, Songwe na Mbeya. Kwa hiyo, nitafika Rungwe na nitafika Tukuyu. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Haonga, swali la nyongeza.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Scheme ya Umwagiliaji ambayo ipo Kijiji cha Mbala Wilaya ya Mbozi, imetengenezwa tangu mwaka 1971 na miundombinu ya scheme hii imeharibika sana na hadi sasa haifanyi kazi. Naomba nijue Mheshimiwa Waziri atakapokuja Songwe yupo tayari kuongozana na mimi kuelekea kwenye scheme hiyo ya umwagiliaji na baada ya hapo sasa Serikali iweze kutengeneza miundombinu miundombinu ya scheme umwagiliaji ili wananchi hao waweze kunufaika na scheme hiyo? (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, nadhani hapo jibu ni fupi kabisa, kwa hiyo kama ulivyojibu lililopita ili tuokoe wakati.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba zipo scheme nydingi ambazo hazifanyi kazi, lakini tumesema mara nydingi kwenye Bunge hili kwamba tumeshatuma watu wanafanya mapitio ya scheme zote ili kuweza kuainisha mahitaji yake. Kwa hiyo, kwenda tu bila kuwa na jibu haisaidii, kwa sababu ameshasema kwamba haifanyi kazi. Kwa hiyo, tunaleta watu wataalam ili waainishe ni vitu gani vinatakiwa vifanyike kwa ajili ya kufanya ile scheme ifanye kazi. Kwa hiyo, naomba tusubiri ripoti ile itakavyoandikwa halafu tutaona hatua za kuchukua. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, swali fupi.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, utaratibu wa kuanzisha miradi ya scheme ya umwagiliaji na kutoimaliza sasa unaonekana kama ni utaratibu wa kawaida, ukiacha kwamba uzalishaji hautafanyika lakini pana pesa ile ambayo ndiyo imeanzisha hiyo miradi, hiyo pesa itapotea. Mfano mzuri ni miradi ya umwagiliaji katika Jimbo la Mtama, katika Vijiji vya Utimbe, Kiwalala na Mbalala ambayo imeanzishwa karibu miaka mitano mpaka saba iliyopita, imeishia katikati na haijamalizwa. Je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kuimalizia miradi hii ili tufaidike na miradi hii? (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ipo miradi mingi ambayo ilikuwa imeanzishwa na haikukamilika. Huko nyuma miradi hii katika Program ya Maendeleo katika Sekta ya Kilimo, sehemu kubwa ya miradi ile ilikuwa inaendelezwa na wafadhili kwa fedha za nje. Sasa tumeona kwamba ni lazima sisi kama Serikali tuwekeze fedha za ndani na kusimamia ili miradi iweze kukamilika na ndio maana tumeunda Tume ya Umwagiliaji ili iweze kusimamia miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuunda Tume hii, mwaka huu tumeamua kwanza kuititia miradi yote na kuainisha mahitaji yake. Kwa hiyo, Serikali itatenga fedha kulingana na yale mahitaji yatakayokuwa yameainishwa ili miradi hii ambayo tumeipanga iweze kutekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kanali Mstaafu, Masoud Khamis, Mbunge wa Mfenesini, sasa aulize swali lake.

Na. 110

**Hitaji la Gari Katika Kituo cha Polisi –  
Mfenesini Zanzibar**

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikitoa ahadi za kutatua tatizo la usafiri kwa Jeshi la Polisi bila mafanikio. Kwa mfano, Kituo cha Polisi Mfenesini, Zanzibar hakina gari la uhakika kwa takribani miaka 10 sasa:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka gari Kituo cha Polisi Mfenesini?

(b) Je, ni lini magari ambayo yamekuwa yakizungumzwa kwa muda mrefu yatawasili nchini ili kuondoa adha ya usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kanali (Mst) Masoud Ali Khamis, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Mfenesini kipo Mkoa wa Kaskazini Uguja katika Wilaya ya Kipolisi Mjini Magharibi A. Mkoa wa Kaskazini Uguja una jumla ya magari 13 ambayo yanatoa huduma za doria na kazi nyingine za Polisi katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Mjini Magharibi ikiwemo Kituo cha Polisi Mfenesini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha Polisi Mfenesini kitapatiwa gari mara baada ya taratibu za upatikanaji wa magari utakapokamilika. Hata hivyo, gari la Mkuu wa Polisi wa Wilaya hutoa huduma pale inapotokea dharura ikiwa ni pamoja na kuwachukua mahabusu waliopo katika kituo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari haya yamekuwa yakiwasili nchini awamu nchini awamu kwa awamu ambapo hadi sasa jumla ya magari 231 yamekwishawasili kati ya magari 777 yaliyokuwa yameagizwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud, swali la nyongeza.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna magari 13 yanatoa huduma za doria katika maeneo hayo. Nataka nimfahamishe tu Mheshimiwa Naibu Waziri, mimi naishi karibu na kituo hiki, hata kilomita moja haitimii. Yameshatokea matukio kadhaa na Askari wanawajibika kuondoka kituoni kwenda kwenye matukio yale wanashindwa kufanya hivyo na wakati mwingine tumekuwa tukitoa msaada wa magari yetu binafsi kuwasaidia. Je, kati ya magari haya 13, kwa nini sasa gari moja lisipelekwe Kituo cha Polisi Mfenesini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa ufahamu wangu mkataba wowote wa kuagiza vifaa vyovoyote vile vya kijeshi ama vya kiraia unakuwa na makubaliano na supplier vitu

vile vitawasili lini. Magari haya tunaambiwa yanakuja kwa awamu na swali lilikuwa yatawasili lini hata kama kwa awamu, je, magari yatawasili lini? (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika majibu ya msingi, kwamba tutapeleka gari katika kituo cha Wilaya cha Mfenesini kwa kutambua kwamba magari haya 13 ya Mkoa na gari ambalo anatumia OCD hayakidhi haja. Nimhakikishie tu kwamba hivi sasa tuna mpango wa kupata magari 50, bahati mbaya hatuna hakika kama yapo magari ya kutosha yenze sifa za kukidhi kuwa magari ya kituo, kwa sababu mengi ya magari ambayo tunatarajia yaje sasa hivi ambayo tayari yameshafika tupo katika mkakati wa kuyatoa mengi ni malori.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ikionekana kwamba magari hayo yanakidhi vigezo vya kuweza kuhudumia Kituo cha Mfenesini, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo chake cha Mfenesini ni moja katika maeneo ambayo yatapata gari hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Tatizo lililopo Mfenesini linafanana kwa ukaribu kabisa na tatizo ambalo lipo katika Mkoa wa Songe na ukizingatia kwamba Mkoa wa Songwe ni mpya na umekuwa na changamoto kubwa sana za kiuhalifu. Changamoto kubwa iliyopo ni suala la usafiri kwa Jeshi la Polisi hususan katika Wilaya mpya ya Songwe. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka magari katika Mkoa wa Songwe hususan katika Wilaya mpya ya Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Mikoa na Wilaya mpya nyangi zina changamoto sio tu za magari pamoja hata na vitendea kazi, ofisi na nyumba. Kwa hiyo, ni kipaumbele cha Wizara yetu kuona kwamba tunapopata vifaa na uwezo wa kuweza kuimarisha vitendea kazi katika maeneo hayo, tunaangalia mikoa hii ambayo ni mipyä ukiwemo Mkoa wa Songwe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, swali la nyongeza.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kituo cha Polisi Himo kinatoa huduma kwa watu zaidi ya laki tano na kipo mpakani na Serikali ilishaahidi hapa Bungeni tangu mwaka 2013 kwamba itapeleka magari mawili (2) mapya kwa ajili ya kutoa huduma kwenye kituo hicho kutokana na umuhimu wake. Hali sasa ni tete sana, kituo kinatumia pipipiki wako kwenye hali mbaya sana. Je, sasa Serikali ni lini kwa dharura itapeleka magari haya mawili waliyoahidi kwa zaidi ya miaka minne (4) katika Kituo cha Polisi cha Himo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbatia kwamba kama ni ahadi ambayo imetolewa na Serikali ya kupeleka gari katika kituo cha Himo, basi nitaifutilia nitakapotoka tu hapa, kujua ni kitu gani kinachokwamisha ahadi hiyo isitekelezwe mpaka leo ili tuone jinsi gani tunaweza tukaitekeleza pale tutakapopata uwezo wa magari ya kutosha tuangalie haraka iwezekanavyo tunaweza viyi kutimiza ahadi hiyo ya Serikali ya muda mrefu.

**MHE. MAGANLAL MEISURIA BHAGWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana umenipa nafasi, Mungu akuweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme jambo moja katika Jimbo langu la Chwaka, hakuna gari katika Jimbo la Chwaka pamoja na Jozani kwa sababu pana bahari na hoteli zipo nydingi sana. Kwa hiyo, wanaweza kuja majambazi, inaweza kuwa ni mambo ya siasa, hivyo ni muhimu sana gari ipatikane haraka kwa watu wangu wa Jimbo la Chwaka pamoja na Jozani, kwa hisani yako. (Makofi/Kicheko)

**NAIBU SPIKA:** Kwa hisani yako Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumelipokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na tutalifanyia kazi. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo sasa aulize swali lake.

Na. 111

#### **Umuhimu wa Kuboresha Vituo vya Afya vya JWTZ**

**MHE. SAADA MKUYA SALUM** aliuliza:-

Vituo vya Afya vinavyomilikiwa na Jeshi la Wananchi vimekuwa vikitoa huduma za afya kwa wananchi wengi na kutopteka na umadhubuti na umakini wa watendaji, wananchi wamejenga imani kubwa juu ya huduma zinazotolewa katika vituo hivyo; hata hivyo huduma hizo zimekuwa zikikabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwemo uhaba wa dawa, Madaktari na vitendea kazi:-

Je, Serikali imeweka mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha kuwa vifaa tiba, dawa na Madaktari vinapatikana ili kutoa huduma bora?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa linaendelea na hatua ya kuboresha huduma za tiba Jeshini, kama ifuatavyo:-

(a) Kuendeleza kuwashawishi wataalam wa tiba wenye sifa kujunga na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kulingana na nafasi za ajira zinazopatikana.

(b) JWTZ limeendelea na utaratibu wa kuwaendeleza Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma kupata elimu katika ngazi mbalimbali zikiwemo Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili kuititia vyuo vyetu vya kijeshi mfano "Military College of Medical Services" pamoja na vyuo vya kiraia nje ya Jeshi. Aidha, Serikali kuititia Wizara ya Afya imeendelea kuwadhamini wataalam wa tiba wanaosomea Shahada ya Uzamili na Uzamivu.

(c) Serikali kuititia Wizara ya Afya imekuwa ikiendelea kutoa ruzuku na kuongeza upatikanaji wa madawa na vifaa tiba.

(d) Kupitia wafadhili mbalimbali mfano Serikali ya Marekani na Serikali ya Jamhuri ya Ujerumani, huduma za tiba zimeendelea kuboreshwa hasa kwa kuongeza miundombinu na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu niliyotoa katika sehemu (a) mpaka (d), Wizara yangu iko katika mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Ni imani yetu kuwa Mfuko huo utakapoanzishwa utaweza kuongeza rasilimali fedha katika utoaji huduma za afya Jeshini. Fedha hizo za ziada zitatumika katika kuboresha miundombinu na upatikanaji wa dawa na vifaatiba hivyo kuboresha huduma za afya kwa Wanajeshi na wananchi wanaotumia vituo vya afya vya Jeshi kupata tiba. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, swali la nyongeza.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; katika mikakati ambayo imeorodheshwa ni kazi gani hasa zimefanyika katika kituo cha Afya cha Jeshi kilichopo Welezo ambacho kinahudumia wananchi wengi na hali yake ni mbaya sana. Kwa hiyo, hii mikakati imeorodheshwa lakini katika mwaka 2016/2017 ni kazi gani hasa zimefanyika katika kituo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; namwomba Mheshimiwa Waziri tukiondoka Dodoma tufuatane, mguu kwa mguu twende katika Jimbo la Welezo tukatembelee kituo hiki cha afya, kipo katika hali mbaya na kinahudumia wananchi wengi na wengi wanakitegemea. Kwa hivyo, akienda akiona utajua sasa ni jinsi gani anaweza kukisaidia. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Katika swali la pili Mheshimiwa Spika alisema kiombwe kibali kwake kwa wanaotaka kuambatana na Mawaziri Majimboni kwao. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu. (Kicheko)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mikakati niliyoielezea kuna baadhi ambayo imeshaanza na kuna baadhi ambayo bado tunategemea itaanza siku za usoni. Lile la Bima ya Afya ambayo kwa kweli tunadhani ndio itakuwa mkombozi wa kuboresha huduma za afya, hilo bado halijaanza, tupo katika mchakato na ni matumaini yetu kwamba likianza fedha nyingi zitapatikana ili kuweza kuboresha vituo hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yale yaliyoanza ni msaada uliotolewa na Serikali ya Marekani na Ujerumani. Tumeshafanya ukarabati na tumenunua vifaa, lakini tumeanza na ngazi za Hospitali za Rufaa za Jeshi. Kwa sababu hata kwenye Jeshi kuna vituo vya afya, hospitali na hospitali kuu. Kwa hivyo, kazi iliyofanyika kwa mfano katika Hospitali Kuu ya Lugalo, kazi zilizofanyika katika Ali Khamis Camp Pemba, kazi zilizofanyika Mwanza na kadhalika ni kubwa na tunajua kwamba kazi hii haijakamilika kwa sababu bado kuna vituo hatujavifikia ikiwemo hicho cha Welezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowenza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tutafika, tunakwenda kwa awamu ili na chenyewe tukiboreshe wananchi pamoja na Wanajeshi waweze kupata huduma nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kutembelea katika kituo hicho, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nipo tayari, nitakapofanya ziara ya eneo la Unguja, basi moja ya kazi zangu itakuwa ni kufuatana naye kwenda kuangalia kituo hicho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuwajengea wanajeshi kituo kizuri cha afya pale Ali Khamis Camp Jimbo la Wawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vitu vingi vya afya vinavyomilikiwa na Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hakuna majokofu ya kuhifadhia maiti, hata kwa Askari wenyewe pale wanapofariki kwa sababu wengine wanakaa mbali sana na maeneo ya mikoa yao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka majokofu katika vituo tofauti vya Afya vya Jeshi ili Askari wenyewe wanapofariki waweze kuhifadhiwa vizuri? Ahsante sana. (Makofu)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba kuna umuhimu wa kuwa na majokofu ya kuhifadhia maiti katika vituo vyetu vya Jeshi, kwa sababu vingi sasa hivi vinatoa huduma ya rufaa na bila shaka ni muhimu kuwa na majokofu hayo endapo itatokea vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swalii la msingi, ni kwamba lazima twende kwa awamu. Tunaanza kwenye vituo vikubwa na kazi hii tumeshaifanya pale Lugalo ni matarajio yetu kwamba kila fedha zitakapokuwa zinapatikana, basi huduma hii tutaiendeleza katika vituo vya chini. Kwa hiyo, nataka nimtoe hofu, jambo hili tunalijua na tutalifanya kazi ili hatimaye vituo hivyo vipate majokofu ya kuhifadhia maiti.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swalii lake.

Na. 112

### Chuo Maalum cha Wataalam wa Vifaa Tiba

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa ujuzi wa kufanya matengenezo vifaa tiba kutokana na ukosefu wa watu wenyewe utaalam huo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwa na chuo maalum kwa ajili ya kufundisha wataalam wa vifaa tiba?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mafunzo ya wataalam wa matengenezo ya vifaa tiba yanatolewa kwenye Vyuo viwili ambavyo ni Dar es Salaam Institute of Technology (DIT) pamoja na Arusha Technical College (ATC). Mafunzo haya yalianza hapa nchini mwaka 2011 kwa kufundisha Stashahada (Diploma) za matengenezo ya vifaa tiba kwa miaka mitatu, jumla ya wanafunzi 32 walihitimu mwaka 2014 ambapo wahitimu 17 walitoka DIT na 15 walitoka ATC. Wahitimu wote hao walipata ajira sehemu mbalimbali nchini. Mwaka 2015, jumla ya wataalam wengine 32 walimaliza mafunzo yao na sasa wanasubiri ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wahitimu wa fani ya ufundi wa vifaa tiba kuanzia mwaka 2016 ni 60. Idadi hii itaongezeka na kufikia wahitimu 85 mwaka 2019. Idadi ya wahitimu wote ifikapo mwaka 2025 inakadiriwa kuwa 1,107 ambayo ni sawa na asilimia 24 ya mahitaji yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maboresho ya utoaji wa huduma za kibingwa hapa nchini kufanywa na sekta ya umma lakini pia na sekta binafsi, hasa katika kuongeza vituo vya utambuzi wa magonjwa ni dhahiri kuwa mahitaji ya wataalam hawa yataongezeka maradufu na hivyo uzalishaji wa wataalam hawa ni kipaumbele kwa Serikali na hivyo, mipango ya kuongeza vyuo vya mafunzo iko bayana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Mwalongo, swalil la nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nina swalil moja tu la nyongeza, lakini naomba nitoe na ushauri kwa Serikali. Kwanza kabisa nitoe ushauri kwamba kuongeza vyuo haitakuwa msaada mkubwa sana, niombe sana sasa Serikali ione umuhimu wa kuboresha mafunzo katika hivi vyuo viwili. Dar es Salaam Institute pamoja na Arusha Technical kwa kuongeza vifaa vya kufundishia vijana hawa na kuboresha ufundi. Kwa sababu Serikali inaposema asilimia 24 itakuwa imefikiwa mwaka 2015 maana yake hali ni mbaya sana. Kwa hiyo niiombe sana Serikali iliangalie hilo iboreshe mafunzo katika vyuo hivi vilivyopo na wafundishe mpaka level ya degree.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo, bado utauliza swalil au unatoa tu ushauri utakuwa umemaliza? Kwa sababu unamaliza muda wako wa kuuliza maswali ya nyongeza.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitauliza.

**NAIBU SPIKA:** Basi ahirisha ushauri, unaweza ukampa Mheshimiwa Waziri baadaye, sasa hivi ni kipindi cha maswali na majibu.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri nimeshaumaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na wataalam hawa kutengeneza vifaa vya tiba, lakini wako wataalam wa kupima kwa kutumia hivi vifaa wajulikanao kwa jina la Radiologists, Halmashauri ya Mji wa Njombe katika Hospitali yake ya Kibena ina wataalam hawa wawili lakini ni wa daraja la pili. Je, Serikali iko tayari kutuletea Radiologist Grade One ili aweze kutumia mashine ambayo Halmashauri tumeinunua pale katika Hospitali yetu ya Kibena?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ushauri wake tumeupokea, lakini kwa sasa tupo katika jitihada za makusudi za kuongeza idadi ya wadahiliwa kwenye fani mbalimbali za Uhandisi wa vifaatiba, lakini pia Serikali kuititia vyuo vyake vikuu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) pamoja na Muhimbili University of Health and Allied Sciences (MUHAS) kwa ajili ya kutengeneza mtaala ambaao utatumika kufundisha hao wanafunzi wa uhandisi kwenye eneo la vifaatiba kwa sababu tunakoelekeea teknolojia ya vifaatiba itaendelea kuongezeka, kukua kwa kasi na tunaendelea kuingiza nchini kama nilivyota maelezo yangu hata jana hapa. Kwa msingi huo, mafundi hawa lazima tuwe nao wa kutosha. Kwa hiyo, tumeona tuanzishe degree ya Uhandisi wa Vifaatiba kwenye Vyuo Vikuu vya Muhimbili pamoja na kile cha Dar es Salaam. Malengo ni hayo ya kukabiliana na mahitaji ambayo yanajitokeza nyakati na nyakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia swali lake la pili kuhusu kupeleka mtaalam wa kupima mionzi (Radiologist) pale Kibena, naomba nilichukue ombi lake na pindi tutakapokuwa tunaajiri wataalam na kuwatawanya kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu tutazingatia ombi la Mheshimiwa Mbunge.(Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Ndoholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 113

**Benki ya Wanawake Kufungua Matawi Nchi Nzima**

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE** aliuliza:-

Mwaka 2007 Serikali ilianzisha rasmi Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) kwa lengo la kuwawezesha wanawake wajasiriamali kupata huduma za kibenki ikiwemo mikopo yenyе riba nafuu, lakini mpaka sasa benki hiyo ina matawi manne tu, mawili yakiwa Dar es Salaam na mengine Mikoa ya Mwanza na Dodoma wakati wanawake wenye uhitaji wa huduma hiyo wako nchi nzima.

Je, Serikali, ambayo inamiliki TWB kwa zaidi ya asilimia 90 inakwama wapi kuiwezesha benki hii ili kufungua matawi kote nchini ili wanawake waweze kunufaika na huduma hizo na hatimaye kujikwamua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Ndoholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa mwaka 2009. Tangu kuanzishwa kwake benki imefanikiwa kuwa na matawi mawili katika Mikoa wa Dar es Salaam na mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa huduma za Benki ya Wanawake Tanzania zinawafikia wanawake waliopo katika mikoa yote hapa nchini. Utekelezaji wa mpango huo unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa mtaji wa benki. Hivyo, katika kuhakikisha azma hii inafanikiwa, benki imekuwa ikipua huduma zake katika Mikoa mbalimbali ya Tanzania kwa awamu kwa kufungua vituo vya kutolea mafunzo na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa benki imeanzisha jumla ya vituo 252 katika Mikoa saba ya Dar es Salaam, Mbeya, Njombe, Iringa, Mwanza, Ruvuma na Dodoma. Kwa mwaka 2017/2018, benki inatarajia kufungua vituo vipyta vya kutolea mafunzo na mikopo katika Mikoa ya Singida, Arusha na Zanzibar. Aidha, katika kipindi husika, kituo cha Dodoma kitaboreshwa na kupandishwa hadhi na kuwa tawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashakikisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali itaendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa mtaji wa benki hii unaimarika ili huduma za Benki ya Wanawake Tanzania ziweze kupatikana katika mikoa yote ya Tanzania. Jitihada hizo ni pamoja na:-

Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wakopaji; kuongeza amana kutoka kwa wateja na wawekezaji binafsi; kuimarisha ubia wa kimkakati na wadau, mfano

African Development Bank pamoja na kuendelea kuajiri wafanyakazi wenye weledi na walio waadilifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe, swali la nyongeza.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa malengo makuu ya kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake ni kumkomboa mwanamke wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Singida. Swali la kwanza, je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha dirisha maalum la wanawake kwenye benki ambazo inamiliki hisa kama NMB ili kuwawezesha wanawake wa Mkoa wa Singida kupata mikopo nafuu wakati Serikali ikiendelea kujipanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa wanawake wengi wamejikita katika shughuli za ujasiriamali lakini hawana dhamana za kukopa; Je, Serikali inatoa maelekezo gani kwa SACCO\$ na benki binafsi ili kuwawezesha wanawake wengi kupata mikopo? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwaka huu akinamama wa Singida wana bahati kwa sababu tunaanza hatua ya awali ya kufungua kituo cha kutolea huduma za Benki ya Wanawake. Singida ni katika mikoa mitatu ambayo tumeamua kuwekeza mwaka huu. Sambamba na mkakati huo tulionao, wazo lake tunalichukua, kwamba Benki yetu ya Wanawake Tanzania iangalie uwezekano wa kufungua madirisha maalum kwenye benki mbalimbali ambazo zipo katika maeneo mengi zaidi nchini. Ni wazo zuri, tunalichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie, teknolojia ambayo imeingia sasa hivi kwenye huduma za kibenki hapa nchini ya kutumia mitandao lakini pia ya kutumia simu za mkononi, nayo itatusaidia kuwafikia Watanzania wengi zaidi na huduma za kibenki na hata huduma za kimikopo huko tunakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tuna management mpya ya *Tanzania Women's Bank* ambayo imeanzisha mazungumzo na wenzetu wa TTCL pamoja na wa Halotel kwa ajili ya kutengeneza mifumo ya kibenki ambayo inatumia simu za kiganjani ili kuwafikia wananchi walio wengi zaidi na mikopo pamoja na huduma mbalimbali za kibenki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu SACCO\$ na benki binafsi; tunazishauri ziendelee kufanya kazi kwa ukaribu na wataalam wetu wa Benki ya Wanawake Tanzania ili waone ni namna gani wanaweza wakashirikiana kwa pamoja kuwashudumia wanawake ambaa ni wajasiriamali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Hivi Serikali ina mpango gani mahsus wa kuwaangalia na wanawake wa vijijini, kwa sababu mipango mingine yote imefeli kwa wanawake wa vijijini kupata mikopo? (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa

Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa yeye pia ni Kada wa Chama cha Mapinduzi, naomba nimkumbushe kwamba kwenye llani ya Uchaguzi pamewekwa maelekezo kwamba kila Halmashauri nchini itenye asilimia tano ya bajeti yake kutoka kwenye Own Source kwa ajili ya kuwakopesha akinamama, huu Mfuko unajulikana kama Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wanawake wote, wakiwemo wanawake wa vijijiini, hata wale anaowapenda sana wa kule Same, nao wanaweza wakatumia fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yetu ssi Waheshimiwa Wabunge ni kuingia kwenye vikao vya Halmashauri wakati tunapanga bajeti na kushiriki kuhakikisha asilimia tano ya akinamama inatengwa, asilimia tano ya vijana inatengwa. Pia tusiishie hapo, pesa zinapopatikana tuziweke pembedi pesa za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wabunge ni Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ambayo huwa inahusika kugawa hizi pesa kwenye vikundi mbalimbali. Kwa hiyo baada ya kuwahamasisha wananchi wetu waombe mikopo hii ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, pia tushiriki kwenye vikao vile vya Halmashauri ambavyo vinagawa pesa hizi kwenye vikundi mbalimbali vya akina mama ili ziwafikie kwa uhakika wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kupitia Benki ya Wanawake tunatengeneza mifumo sasa ambayo itawafikia Watanzania popote pale walipo, hata wa kijijiini, sasa hivi matumizi ya simu ni kwa zaidi ya watu milioni 36 hapa nchini, kwa hiyo njia hii itawafikia watu wengi zaidi hapa nchini kwetu. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, Mbunge wa Geita Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Lyimo.

Na. 114

**Agizo la Kuwakamata Wanawake Wanaojiuba**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU)** aliuliza:-

Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto hivi karibuni alitoa agizo la kuwakamata wanawake wanaojiuba:-

Je, zoezi hili limefanikiwa kwa kiasi gani nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kumekuwa na vitendo vya wanawake kuijuza katika sehemu mbalimbali nchini, hasa maeneo ya mijini. Tatizo hili limekuwa kubwa zaidi katika Mikoa na Miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa vifungu vya Sheria Na. 146A, 176(a) na 176A vya Sheria ya Makosa ya Jinai, (Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002), kitendo cha mwanamke kuishi akitegemea kipato chake au sehemu ya kipato chake kutohana na ukahaba ni kosa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, katika kuhakikisha kuwa sheria hii inatekelezwa ipasavyo, viongozi katika mikoa mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Dar es Salaam wamekuwa wakiwakamata na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria wanawake wanaojiuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kufanya operesheni ya kuwabaini na kuwakamata wamiliki wenye madanguro yanayotumiwa na makahaba hao. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutahakikisha wanawake wanaojihusisha na biashara hii wanaendelea kukamatwa ili kulinda heshima, utu na hadhi ya wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nitumie fursa hii kuwataka wanawake wanaofanya biashara hii kuacha mara moja na kutafuta shughuli nyingine ya kujipatia kipato cha halali. Pia napenda kuwaasa wanaume kuacha kujihusisha katika biashara hii yenye madhara kwa familia zao kiuchumi na kijamii, kwani wao wakiacha wanawake hawa watakosa soko. Aidha, kwa mwanaume kuwa mteja wa biashara hii nalo pia ni kosa kisheria. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzan Lyimo, swalii la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa sababu nilikuwa nimefikiri atazungumzia wanawake tu kwa kuwa hii biashara ni ya watu wawili. Hata hivyo, nina swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa, pamoja na kwamba kunakuwa na biashara hiyo ya wanawake na wanaume, lakini pia sasa hivi kuna biashara ya *homosexuals*, wanaume peke yao au *lesbians*; je, hawa wanachukuliwa hatua gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hiyohiyo niliyoisema wakati natoa majibu ya msingi hapa inakataza pia vitendo vya watu wa jinsia moja kufanya mapenzi kinyume cha maumbile. Pia inakataza hata, kwa mfano kwa mwanaume kufanya vitendo ambavyo vinaashiria kwamba ni vya jinsia ya kike, yaani kufanya mambo ya kike wakati wewe ni mwanaume. Sheria hiyo inakataza na inayajinaisha na kuna adhabu kali ambayo inatolewa na sheria hiyo, ni zaidi ya miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumekuwa tukipambana kwa nguvu zetu zote na makundi haya ambayo yamekuwa yakishiriki kwenye vitendo vya mapenzi ya jinsia moja ama kuyahamasisha ama kuyahalalisha ama kuyafanya yaonekane ni vitu vya kawaida kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu tulienedesha operesheni kubwa ya kudhibiti vitendo hivi lakini pia hata taasisi ambazo zilionekana zina mwelekeo wa kutekeleza afua mbalimbali za kinga kwenye sekta yetu ya afya tumezifuta, tumezibadilisha. Hata miongozo ambayo iliruhusu baadhi ya afua zinazohusiana na kupunguza maambukizi kutoka kwa watu wanaofanya mapenzi ya jinsia moja nayo tumeibadilisha, kwa hiyo tuko vizuri. Watakaofanya hivyo watakatamatwa na Jeshi letu la Polisi na watachukuliwa hatua za kisheria.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, maarufu kama Mheshimiwa Bwege, tafadhali.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika Tulia uliyetulia.  
(Makofi/Kicheko)

Na. 115

### **Ujenzi wa Barabara ya Singino/Kivinje – Kilwa**

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA** aliuliza:-

Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Singino/Kivinje maarufu kama Barabara ya Kwa Mkocco ni ahadi ya Serikali iliyotolewa na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, karibu miaka 10 iliyopita. Aidha, kwa kipindi chote cha miaka 10 ujenzi wa barabara hiyo umekuwa wa kususua ingawa barabara hiyo ni kiunganishi kwa wananchi hasa wagonjwa wanaokwenda kutibiwa hospitali ya wilaya:-

(a) Je, ni nini kauli ya Serikali ya Awamu ya Tano juu ya ukamilishwaji wa ahadi hiyo?

(b) Je, Serikali inatoa maelezo gani kwa wananchi juu ya kucheleta kukamilishwa kwa ujenzi wa barabara hiyo kwa kipindi cha miaka 10 sasa?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Singino/Kivinje – Kilwa ni barabara inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Katika mwaka 2012, Mheshimiwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne aliahidi kutenga fedha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ili barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ilisaini mkataba na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 1.478. Hata hivyo, mradi huo haujakinika na mkandarasi amekimbia eneo la mradi. Wakati wa ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliagiza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Lindi, kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya mahitaji ya fedha zinazotakiwa ili kuendelea kujenga kwa kiwango cha lami barabara hii yamefanyika na ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hii unatarajiwa kuanza pindi fedha zitakapopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Bungara, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa jibu lililotolewa na Mheshimiwa Waziri. Hata hivyo, namwomba sana, kwa kuwa Mheshimiwa Rais Magufuli ameagiza hii barabara ijengwe na mpaka sasa hivi anasema kwamba wanatafuta fedha ili ijengwe, naomba sana waitafute hiyo fedha barabara hiyo ijengwe. Pamoja na hilo, nataka niulize swali la nyongeza; kwanza; je, tathmini hiyo ni shilingi ngapi katika barabara hiyo iliyotathminiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; katika kampeni ya mwaka 2015, Rais Dkt. Magufuli alipokuja Kilwa aliwaahidi watu wa Kilwa kama atashinda Urais atajenga kilometra tano katika Mji Mdogo wa Kilwa Masoko. Sasa pamoja na kwamba ahadi za Rais hizi hazitekelezwi kwa

wakati. Je, ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa sababu Urais alishaupata, na yule Bwana akisema jambo basi linakuwa hivyohivyo anavyosema. Je, ni lini itatimizwa ahadi hii ya kilometra tano katika Mji wa Kilwa Masoko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wetu wa TANROADS walikwenda kufanya tathmini ya barabara hiyo na tukagundua kwamba inahitajika takribani bilioni tatu kwa ajili ya kukamilisha barabara hiyo. Mwezi huu uliopita tu Halmashauri zilipelekewa takribani milioni 400, sasa tunaamini kazi iliyopo mbele yetu ni kutafuta bilioni 2.6 kwa ajili ya kukamilisha barabara hiyo. Mheshimiwa Rais alinipa jukumu hilo na nitahakikisha kwamba pesa hizo tunazitafuta ili barabara hiyo iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni kuhusu ujenzi wa kilometra tano Mjini Kilwa Masoko. Ahadi zote alizotoa Mheshimiwa Rais tumezichukua na tunazifanya kazi na tutahakikisha hivi karibuni tutaanza kuzitekeleza moja baada ya nytingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara inayotoka Lushoto kwenda Mlalo, kilometra 42, ambayo ndiyo inayounganisha Majimbo haya imekuwa ikijengwa na Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa kilometra mbili mbili kwa kila mwaka. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuitengea fedha barabara hii ili iweze kurahisisha mawasiliano kati ya Mlalo, Mtae na Lushoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Lushoto – Mlalo ni barabara ambayo inahudumiwa na TANROADS Mkoa wa Tanga na inapitika siku zote, mwaka mzima, haina matatizo makubwa. Kazi iliyopo mbele yetu sasa hivi ni kutafuta fedha ili tufanye feasibility study na detailed engineering design ili huko baadaye tuweze kutafuta pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Shangazi kwamba, tutakaa pamoja tutazungumza ili kuhakikisha tunampa mpango mzima ambao tutaweza kuutekeleza ili kuhakikisha barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 116

#### **Utekelezaji wa REA Awamu ya II – Bagamoyo**

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA** aliuliza:-

Katika Mradi wa REA II, Jimbo la Bagamoyo lilipewa vijiji 10 tu na bado utekelezaji wake unasuasua na uko nyuma ya ratiba:-

Je, ni lini miradi ya umeme kwa Vijiji vya Kongo, Kondo na nyongeza ya Matimbwa itakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Shukuru Jumanne Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijiini (REA) ilikamilisha kupeleka umeme vijijiini kupitia Mradi wa REA Awamu ya Pili ikiwemo Wilaya ya Bagamoyo mwezi Desemba, 2016. Kazi ya mradi huo katika Wilaya ya Bagamoyo ilijumuisha ujenzi wa njia kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 80.13, ujenzi wa njia kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometra 106.67 pamoja na ufungaji wa transforma 41, kazi nyingine ilikuwa kuwaunganisha wateja wa awali 2,066 na ghamrama za utekelezaji wa mradi zilikuwa shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya Kijiji cha Matimbwa iliyobaki kupatiwa umeme pamoja na vijiji vingine ikiwemo Kondo vitafikishiwa umeme kupitia Mradi wa REA Awamu ya Tatu iliyoanza mwezi Juni, 2017 utakaokamilika mwaka 2020/2021.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yenye kutia moyo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza; nilijulishwa na uongozi wa REA kwamba Vijiji vya Kongo na Kondo ambavyo havikutekelezewa miradi yake katika awamu ya pili vimeingizwa kwenye orodha ya miradi ya nyongeza kwenye REA-III ambayo imeombewa kibali kwa ajili ya utekelezaji. Sasa swalii; je, lini kibali hicho kitawezeka kutolewa ili miradi hiyo itekelezwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kufuatana na orodha ya miradi ya REA Awamu ya Tatu kwenye Jimbo la Bagamoyo, vijiji vingi katika Kata za Fukayosi, Makurunge, Mapinga, Kerege na Zinga havitopata umeme. Je, Serikali ina mkakati gani kuweza kuvipatia umeme vitongoji hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Dkt. Kawambwa kwa juhudzi zake anavyofuatilia mahitaji ya umeme kwa wananchi wa Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyotaja, Vijiji vya Kondo, Kongo, Matimba pamoja na Fukayosi kimsingi vilishapata approval na viko kwenye REA awamu ya tatu hii inayoanza sasa hivi. Naomba nimhakikishie kwamba katika shule yake ya sekondari aliyojenga Fukayosi kwa wafadhili, tayari wiki ijayo wanafanya survey ili ianze kupelekewa umeme katika awamu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji viliviyobaki ambavyo amevitaja; Mapinga, Kerenge pamoja na maeneo ya Zinga ambavyo ni vijiji 22, navyo vitaanza kupelekewa umeme kuanzia mwezi Machi, 2019 na kufikia mwaka 2020 vyote vitakuwa vimeshapata umeme.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mgumba, swalii la nyongeza.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa matatizo yanayowakabili wananchi wa Bagamoyo yanafanana kabisa na ya Morogoro Kusini Mashariki. Kwenye mipango ya Serikali ya REA awamu ya tatu, Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki tumepata vijiji saba tu na kuacha vijiji 47 kati ya vijiji 64 ambavyo vyote havina umeme katika Kata za Tegetero, Kibuko, Tomondo, Maturi, Mkulazi na Seregeti. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupeleka umeme katika huu mradi wa REA awamu ya tatu, katika Kata hizo na vijiji vyake vyote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge anavyosema. Kwanza nimpongeze, nilipokuja kuzindua Morogoro tulishirikiana na Mheshimiwa Omari na nilimwambia alete vijiji vyake tuviboreshe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tumeshafanya mapitio siyo vijiji saba vinavyopelekewa umeme raundi ya kwanza bali ni vijiji 14. Hata hivyo, vile vijiji vingine 47 alivyotaja basi tutakaa tuvipitie, lakini vyote vitapatiwa umeme kwenye raundi inayofuata itakayoishia mwaka 2021.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 117

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Mradi wa Umeme Kibaha Mjini**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Mradi wa umeme wa 400KV wa kutoka Kinyerezi hadi Arusha ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi na Taifa letu; kuanzia mwaka 2015 wananchi wa maeneo ya Kibaha Mjini ambako mradi huu unapita wamechukuliwa maeneo yao na yalifanyiwa uthamini kwa ajili ya wananchi kulipwa fidia:-

Je, ni lini fidia hii italipwa kwa wananchi walioathirika na mradi huu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) inatekeleza mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Arusha. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 400 yenye urefu wa kilometra 600, pamoja na kilometra 40 kutoka Kibaha hadi Zinga na kilometra 60 kutoka Segera hadi Kange (Tanga).

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu pia unahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika maeneo ya Chalinze, Segera, Kange, pamoja na Zinga (Bagamoyo).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015 kazi ya uthamini wa mali za wananchi kutoka Kibaha hadi Chalinze ilifanyika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Taratibu za kulipa fidia zimekamilika na jumla ya shilingi bilioni 21.56 zitahitajika kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi 855. Maeneo yatakayofidiwa ni pamoja na Kibaha Mjini, Kibaha Vijiji, Bagamoyo pamoja na Kisarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya fidia yataanza mara tu uhakiki utakapokamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Koka swali la nyongeza.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Nabu Spika, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa jitihada kubwa ya kusambaza umeme. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka mradi huu ulipoanza na wananchi kufanyiwa tathmini ni takribani miaka mitatu na wananchi hawa wameacha shughuli zao za maendeleo na hawana fedha kwa ajili ya kuanzisha shughuli nyingine ya maendeleo. Ni lini sasa Serikali itaanza kulipa fidia hii ili wananchi wajiandae kwa ajili ya kuwa na shughuli za maendeleo mbadala katika maeneo mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; katika mradi wa umeme REA III, Vijiji vya Jimbo la Kibaha Mjini ikiwa ni pamoja na Mkombozi, Lumumba, Kalabaka, Saeni, Jonuga, Mbwawa, Miomboni, Madina, Mbwate, Visiga, Viziwaziwa, Mtakuja, Maili 35 na Kumba vimeondolewa katika utaratibu mzima wa REA III na katika kufuatilia kwangu hatujapata majibu ni utaratibu gani utatumika kuipatia Mitaa hii umeme kama ilivyokuwa imepangwa na wananchi wana mtafaruku mkubwa. Je, Serikali sasa ina mpango gani mbadala kuhakikisha mitaa hii yote inaendelea kupata umeme kama tunavyojua umeme ni uchumi na maendeleo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Koka hongera sana katika kufuatilia masuala ya fidia. Mmefika hatua nzuri kwa sababu ya jitihada zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba katika maeneo yaliyofanyiwa tathmini kama nilivyoeleza kwenye swalii langu na jibu langu la msingi kwamba taratibu zimeshakamilika na ni matarajio yetu mwisho wa Desemba na mwanzo wa Januari mwakani, malipo yatakuwa yameshaanza kutoka. Kwa hiyo, wananchi wa maeneo yale wategemee fidia katika kipindi hicho, lakini kama nilivyosema, taratibu za uhakiki zimeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii lake la pili; nitumie nafasi hii kusema kwamba yako maeneo ambayo kwa kweli ni mitaa ingawa katika hali ya kawaida inaonekana kama vijiji. Maeneo haya ambayo yako mjini kwa sababu miradi ya REA inakwenda vijijini, uko mradi unaoitwa *urban ratification* ambao katika Wilaya ya Kibaha hasa Mjini na maeneo ya jirani yatapelekewa umeme kupitia mradi huu. Mheshimiwa Koka kwa bahati nzuri sana, katika maeneo ya Lumumba, Mtakuja na Viziwaziwa ziko *transformer* 11 zimetengwa kwa ajili yakupelekewa umeme katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na.118

#### Changamoto Zinazowakabili Wakulima wa Lindi

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE** aliuliza:-

Asilimia 85 ya wananchi wa Mkoa wa Lindi ni wakulima wa korosho, ufuta na mbaazi. Pamoja na juhudii kubwa za uzalishaji, wakulima hao wamekuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali za ukosefu wa masoko, ucheleweshwaji wa pembejeo na kuongezeka kwa ushuru:-

(a) Je, ni lini Serikali itawashirikisha wakulima hawa katika upangaji bei hasa zao la korosho badala ya Bodi pekee ambayo inapanga bila kuangalia gharama halisi za kulima?

(b) Je, ni lini Serikali italianzisha tena soko la uhakika la mazao ya wakulima baada ya kulifunga lile la awali Wilayani Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lathifah Hassan Chande, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikishwaji wa wakulima na wadau wa korosho katika upangaji wa bei ya korosho na mjengeko wa bei ni kwa mujibu wa Sheria ya Korosho ya Mwaka 2009. Kwa hali hiyo, kabla ya kuanza msimu mpya wa soko la korosho, wadau hukutana ambapo Wawakilishi wa wakulima huwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote na kukubaliana kuhusu bei dira. Bei hii huzingatia wastani wa gharama za uzalishaji wa korosho ghafi shambani na hali ya soko la nje kwa kipindi kisichopungua miezi sita iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya kuweka bei dira ni pamoja na kumwezesha mkulima kuhimili ushindani wa soko kwa kuwa na uhakika wa kurudisha gharama zake za uzalishaji wa korosho ghafi katika msimu husika, pia juu yake huwekwa asilimia 20 ya faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa kupata bei dira ya korosho hufanyika baada ya utafiti wa kina wa gharama za uzalishaji wa korosho na kumsaidia mkulima kupata bei yenye maslahi sokoni kuititia mfumo wa soko wa stakabadhi ghalani. Kwa mantiki hiyo, upangaji wa bei dira ya korosho unashirikisha wakulima na huzingatia gharama halisi za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha masoko ya mazao mbalimbali kadri itakavyoonekana inafaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lathifah Chande, swali la nyongeza.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali ilisema kwamba itagawa sulphur bure na matokeo yake sulphur iliyogaiwa, nyingi ilikuwa ni feki na nyingine ilikuwa imeshapitwa na muda, yaani ime-expire. Hii inaweza kupelekea kuharibu zao hili la Korosho. Sasa Je, Serikali ikiwa kama mdhibiti, ilikuwa wapi mpaka hii sulphur ikaweza kuingia nchini na hadi kumfikia mkulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba, sasa hivi Mkao wa Lindi wamelima kwa wingi zao la choroko na mbaazi ambalo wamekosa soko hadi kupelekea gunia moja la kilo 100 kuuzwa kwa Sh.15,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo miaka ya nyuma, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Exchange Commodity ambapo ilikuwa na mpango wa kuanzisha Exchange Commodity Market na mpaka dakika hii tayari Ofisi kwa ajili ya Exchange Commodity Market imepatikana na hadi savers zimekuwa set up lakini hakuna operation zozote zinazoendelea; kitu ambacho soko hili la Exchange Commodity lingeweza kuwasaidia wakulima waweze kupata soko la uhakika kwa ajili ya mazao mbalimbali. Sasa je, Serikali ina mpango wa kuanza lini operations katika Commodity Exchange Market? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na viuatilifu au sulphur feki au iliyopitwa na wakati, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge

pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba hakuna sulphur feki wala iliyopitwa na wakati ambayo imesambazwa kwa wakulima. Naomba yejote mwenye ushahidi wa mkulima mmoja tu ambaye ameuziwa au amepewa sulphur feki au ambayo imepitwa na wakati anipe ushahidi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia kwamba hakuna sulphur feki wala ambayo imepitwa na wakati ambayo imesambazwa kwa wakulima. Kilichotokea katika taarifa zile mlizoona kwenye vyombo vya habari ni kwamba kulikuwa na sulphur ambayo iko kwenye maghala ambayo imepitwa na muda, ime-expire lakini haikuwa kwa ajili ya kugawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la commodity exchange, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba utaratibu wa commodity exchange hautafuti soko, yaani siyo kwamba ukishatumia commodity exchange basi unakuwa na uhakika wa soko. Kama soko halipo ni kwamba halipo tu. Commodity exchange haina tofauti kimsingi na utaratibu wa sasa tunaotumia wa stakabadhi ghalani. Tofauti yake kidogo tu ni kwamba yenyewe inatumia teknolojia zaidi, lakini kama hakuna mnunuzi hutapata kwa kutumia commodity exchange.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimhakikishie kwamba Serikali kwa sasa imejivekeza zaidi katika kuimarisha utaratibu tulionao wa stakabadhi ghalani kwa sababu ili tuweze kufikia kwenye commodity exchange tunahitaji vitu vingi. Tunahitaji kuwa na maghala ambayo ni ya kisasa zaidi, tunahitaji teknolojia, tunahitaji kuweza kuzalisha kwa utaratibu unaotakiwa na masoko ya nje lakini vilevile tunahitaji wakulima wetu waweze kuzalisha kwa viwango vile ambavyo vinahitajika. Kwa hiyo, kwa sasa jitihada ya Serikali siyo kwenye commodity exchange, tutaelekea kule, lakini kwa sasa tunaweka nguvu nydingi kwenye utaratibu wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta soko kwa ajili ya mazao ya mikunde. Changamoto iliyotokea ni kwamba India ambayo ndio nchi inayonunua mazao ya mikunde, kwa mwaka huu wana ziada ya asilimia 30 na ndio maana mbaazi zetu, dengu zetu na choroko zimepata changamoto. Hata hivyo kwa kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kununua mbaazi za wakulima, lakini huko mbele ya safari tunagemea tuanze kuuza zao hilo la mbaazi kwa utaratibu wa stakabadhi ghalani tukiamini kwamba kuuza kwa pamoja kutasaidia bei iwe nzuri zaidi. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swali la mwisho. Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Mbunge wa Morogoro Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 119

#### Kulifufua Shirika la Uvuvi-Tanzania (TAFICO)

**MHE. PROSPER J. MBENA** aliuliza:-

Wakati wa mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi tarehe 22 Mei, 2017, Bungeni, Wabunge wengi walieleza umuhimu wa Serikali kuongeza juhudzi za uvuvi kwenye Bahari Kuu na kuitaka Serikali kununua meli kubwa za kuvua samaki kwenye Bahari Kuu:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza sababu zilizofanya Shirika la Uvuvi la Tanzania (Tanzania Fisheries Company-TAFICO) lishindwe kuendelea na biashara ya uvuvi wa Bahari Kuu?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulifufua Shirika hilo la TAFICO?

(c) Je, miundombinu iliyokuwepo ya uvuvi kwa ajili ya TAFICO ikiwa ni pamoja na meli, dry dock na zana nyingi za uvuvi ambazo zilijengwa na kulipiwa na Serikali ya Japan ipo katika hali gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, Morogoro Kusini, lenye vipengele (a), (b) na (c), Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, liliokuwa Shirika la Uvuvu Tanzania (*Tanzania Fisheries Corporation - TAFICO*) lilianzishwa kwa Sheria ya Makampuni ya Umma Na. 17 ya mwaka 1996. Lengo la kuanzishwa kwa TAFICO lilikuwa ni kuendesha shughuli za uvuvi kibiashara katika maji ya ndani na siyo uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1996, Serikali ilitoa tangazo Na. 322 kuhusu kurekebisha Mashirika ya Umma ili yaweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi ambapo TAFICO ilikuwa ni mionganini mwa mashirika yaliyotakiwa kubinafsishwa au kufanyiwa marekebishi. Kwa msingi huo, shughuli za Shirika la TAFICO liliwekwa chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) kwa ajili ya taratibu za ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu wa kufufua TAFICO ili Sekta ya Uvuvu iweze kuchangia ipasavyo katika ajenda ya uchumi wa viwanda. Hivyo Wizara imekamilisha waraka wa Baraza la Mawaziri kwa ajili ya mapendekezo ya kutunga Sheria mpya ya Shirika la Uvuvu Tanzania. Suala hili linafanyika kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam ili kuhakikisha wananchi wananufaika na rasilimali za uvuvi zilizopo ikiwa ni pamoja na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya sera ambapo Serikali ilijitoa kufanya shughuli za moja kwa moja za uzalishaji na biashara, Serikali kupitia Msajili wa Hazina iliuta mali za TAFICO zinazohamishika zikiwemo meli na mitambo ya barafu mwaka 2008 na kubakiza mali zisizohamishika yakiwemo majengo ambayo yamekarabatiwa na sasa yanatumika kama Ofisi za Serikali na matumizi mengine. Aidha, kutokana na kukaa muda mrefu bila kutumika na athari za mvua za *Elnino*, Dry Dock imechakaa na imezama upande mmoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prosper Joseph Mbena, swali la nyongeza.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nashukuru majibu ya Serikali hasa kwa kubaini umuhimu wa kulirudisha hili Shirika la TAFICO kufanya uvuvi hasa kwenye bahari kuu, nadhani wamechukua ushauri wetu, naomba kuwapongeza. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uvuvi ni sekta muhimu sana hasa katika sera hii ya Serikali ya uchumi wa viwanda: Je, ni lini Serikali itasaidia Jimbo la Morogoro Kusini kuleta wataalam wake kufanya utafiti kwenye mito mikubwa yenye utajiri mkubwa wa samaki na dagaa ili nao waweze kuchangia kwenye uchumi huo? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lake ni kwamba, Serikali iweze kupeleka wataalam Jimboni kwake wakafanye utafiti. Naomba nilichukue tukaliangalie ndani ya Wizara ili ikiwezekana wataalam waweze kwenda kule.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Tunaleta matangazo ambayo tunayo kwa siku ya leo:-

Tangazo la kwanza linahusu wageni waliopo Bungeni. Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge tutaanza na hao. Kundi la kwanza ni wageni nane wa Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Ikupa Allex amba ni viongozi wa Chama cha Wasioona Tanzania, wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho Ndugu Luis Benedicto. Karibuni sana. (Makofi)

Tunaye pia Mgeni wa Mheshimiwa Engineer Stella Manyanya ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na huyu ni Diwani kutoka Kata ya Kihagarasi, Nyasa. Huyu ni Mheshimiwa George Ndimbo. Karibu sana. (Makofi)

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Willy Qambalo amba ni viongozi wa Vijiji vya Lositete na Endamaga kutoka Karatu Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Ally Baiko. Karibuni sana. (Makofi)

Wengine ni Wageni tisa wa Mheshimiwa Angelina Mabula amba ni viongozi na Wajumbe wa *The International Evangelical and Good Samaritan Ministries* kutoka llala Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Bishop Bajuta. Karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Kundi la kwanza ni wanafunzi 107 na Walimu sita kutoka Shule ya Sekondari ya Mtakatifu Francis Waasisi iliyopo Kongwa Mkoani Dodoma. Karibuni sana. (Makofi)

Vile vile tunao wageni 56 kutoka Chuo cha St. Gabriel Technical School kilichopo Mkoani Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Margret Sitta ambaye ni Mwenyekiti wa TWPG; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kama mliviotangaziwa jana, anawakumbusha kwamba Wenyeviti wa Kamati za Bunge na Wajumbe wa Kikundi cha Lishe wahudhurie semina katika ukumbi wa Morena mara baada ya Bunge kuahirishwa. Kwa hiyo, wanawake wote, Wenyeviti wa Kamati na pia Wajumbe wa Kikundi cha Lishe, wanaombwa wahudhurie semina hiyo mara Bunge litakapoahirishwa. (Makofi)

Tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa Bunge Sports Club, Mheshimiwa William Ngeleja; anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo asubuhi kwenye Uwanja wa Jamhuri kulikuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa miguu katika ya Bunge Sports Club na Muungano Jogging Veterans na matokeo ya mechi hiyo, Bunge lilishinda goli moja na Muungano waliambulia patupu. Goli hilo la pekee lilitifungwa na mchezaji mahiri, Mheshimiwa Cossato Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini. Ahsanteni sana Bunge Sports Club (Makofi)

Tangazo lingine linatoka Idara ya Shughuli za Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa mara baada ya shughuli za Bunge kuahirishwa, mpite katika eneo la mapokezi kwa ajili ya kuchukua Kamusi Kuu ya Kiswahili. Hili ni muhimu sana Waheshimiwa kwa sababu wote bado tunajifunza matumizi ya lugha. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mapema wiki iliyopita Mheshimiwa Spika alikuwa ameombwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kupeleka jambo ambalo yeye alikuwa amelieleza kwa kifupi (sina haja ya kulirudia) kwenye Kamati inayoshughulika na Mambo ya Ulinzi na Usalama na Mambo ya Nje.

Sasa kwa utaratibu wa Kikanuni, Mheshimiwa Spika alilipeleka jambo hilo na Kamati ilipaswa kumtaarifu Spika kwamba imekamilisha kazi. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Spika aliahidi

jambo hilo litafanywa leo na kwenye Order Paper yetu hatunalo, tumsikie Mwenyekiti kabla hatujaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wiki iliyopita siku ya tarehe 8 Septemba, siku ya Ijumaa, Mheshimiwa Spika aliiagiza Kamati yangu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kutafakari hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Bashe kuhusu hali ya usalama nchini pamoja na usalama wa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hiyo tulitakiwa tuiwasilishe kabla ya kuahirishwa Bunge hili siku ya leo, lakini kutoptana na unyeti na kazi ya shughuli hiyo na umuhimu wa taarifa hiyo, tulishindwa kuikamilisha katika kipindi hiki kwa sababu muda wenyewe ni mdogo sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, endapo utaridhia, tunakuomba uruhusu Kamati hiyo iweze kuendelea na kazi hiyo kuanzia kesho na tunahakikisha kwamba tutakamilisha kabla hatujasambaratika kurudi Majimboni kwetu. Tunakuahakikisha kwamba mara itakapokamilika, tutaitela mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijazungumzia jambo ambalo limezungumzwa na Mwenyekiti, nimeletewa ujumbe hapa na Mheshimiwa Susan Lyimo akisikitika kuhusu wageni wake ambao hajawataja ni akina nani? Wageni wa Mheshimiwa Susan Lyimo popote walipo, karibuni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Susan, siku nyingine ni afadhali uandike, kwa sababu ningepata nafasi ya kuwataja hao ni akina nani.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba yetu, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosughulikia Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ametoa maelezo kwamba Kamati inahitaji muda zaidi. Sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taratibu zetu zilivyo, Spika aandikiwe na kwa sababu mimi ni mshauri wake, nitamshauri ili ombi hilo aweze kuliridhia.

Kwa hiyo, barua iandikwe mapema ili Waheshimiwa Wabunge waweze kutangaziwa juu ya majibu ya hiyo barua atakayoandikiwa Mheshimiwa Spika. Ndiyo utaratibu wetu huo. Kwa hiyo, hiyo barua ipelekwe mapema ili Waheshimiwa Wabunge watangaziwe kabla hawajatawanyika, nini kitakachoendelea.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu!

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, naomba ukae. Katibu.

**DKT. THOMAS KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:**

#### MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017  
(The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017)**

**Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania wa Mwaka 2017  
(The National Shipping Agencies Bill, 2017)**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali  
(No. 4) wa Mwaka 2017 [The Written Laws Miscellaneous  
Amendments] (No. 4) Bill, 2017]**

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumeletewa Miswada ya Serikali ambayo imeshasomwa na kwa hivyo itapelekwa kwenye Kamati zinazohusika ili utaratibu wetu wa Kibunge uweze kuendelea. Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika ataupeleka kila Muswada katika Kamati inayohusika ili Waheshimiwa Wabunge tupate fursa ya kushiriki katika zoezi zima la kutunga Sheria hizi.

Baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:**

**TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE**

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa Nane wa Bunge sasa zimekamilika. Shughuli hizo ni Kiapo cha Uaminifu, Maswali, Miswada ya Sheria ya Serikali, Maazimio na Hoja za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Katibu kwa Taarifa hiyo. Tunaendelea. Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:** Hoja ya Kuahirisha Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Spika ataingia sasa kwa ajili ya kuendelea na utaratibu unaoendelea.

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

**HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE**

**SPIKA:** Hoja ya Kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tafadhalii.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tarehe 5 Septemba, mwaka huu wa 2017, ndiyo siku tulianza Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu na leo tunafikia tamati. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwa amani, salama, utulivu, afya na uzima.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii ya awali kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa hekima, busara na uwezo mkubwa wa kuliongoza Bunge hili ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge watakulaliana nami kwamba kwa mara nyingine ushuhuda huu ni dhahiri na umejidhihirisha wazi katika kikao

hiki ambapo mmeongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuendelea kuonesha ukomavu wa kisiasa kwa kuwa wavumilivu sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri pamoja na michango yenu mizuri ya maoni na ushauri tuliuopokea wakati wa mijadala ya hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiendelea na kikao hiki cha Bunge, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na wananchi tunaowawakilisha katika Majimbo yetu walipata misiba ya ndugu, jamaa na marafiki. Nitumie nafasi hii kuwapa pole wote waliofikwa na misiba hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kama ambavyo wote tunakumbuka mnamo tarehe 7 Septemba, mwaka 2017 tulipata taarifa ya tukio la kusikitisha lilitokoa hapa Dodoma la mashambulizi ya kupigwa risasi kwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Tundu Antiphas Lissu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge pamoja na wananchi mbalimbali nchini kote kwa kumpa pole kwa majeraha na maumivu makubwa aliyoyapata na tunamwombea apone haraka na kurejea kuungana na familia yake, lakini pia nasi hapa Bungeni kwa shughuli za Bunge. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, natumia nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa pole nyngi kwa Meja Jenerali Mstaafu, Vicent Mritaba kutokana na tukio la kushambuliwa kwa risasi siku ya Jumatatu tarehe 11 Septemba, 2017, nyumbani kwake ambaye bado anaendelea na matibabu kwenye Hospitiali yetu ya Lugalo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inalaani vitendo hivyo na matukio hayo ya kinyama. Ni mwezi na nusu sasa tumeanza kuanza kuona utulivu kufuatia vifo vya raia na Askari wetu wa Jeshi la Polisi waliouawa kikatili huko maeneo ya Mbagala, Dar es Salaam, Mkuranga, Wilaya ya Rufiji na Kibiti, Mkoani Pwani.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kusisitiza kwamba kwa matukio haya Serikali haitafumbia macho na tayari vyombo vya dola vimeagizwa kuhakikisha kwamba vinawatafuta kwa mbinu zote wale wote waliohusika katika vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, nirejee kuwasihii Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wote mwendelee kuvuta subira wakati Serikali na vyombo vya dola vinashughulikia matukio haya kwa umakini mkubwa. Jambo la msingi hapa ni kwamba kila mmoja wetu adumishe hali ya ulinzi na usalama nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu liliwaapisha Waheshimiwa Wabunge wapya nane wa Viti Maalum walioteuliwa hivi karibuni. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote hao, amba ni Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Rukia Ahmed Awadh, Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mheshimiwa Sonia Juma Magogo, Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir na Mheshimiwa Rehema Juma Migila. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Septemba, 2017 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Jaji Profesa Ibrahim Hamis Juma kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kupitia Bunge lako Tukufu nimpongeze Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwake katika kuongoza mhimili wa Mahakama. Aidha, nampongeza sana Jaji Mkuu Mstaafu Chande Othman kwa kazi kubwa na nzuri aliyofanya katika kipindi chake cha uongozi wa mhimili huo, hususan kuweka misingi imara ya mhimili wa Mahakama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya kawaida na ya msingi yapatayo 119 na maswali ya nyongeza 283 na kujibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili miswada mitatu na maazimio manne. Vilevile, Bunge lako Tukufu lilipokea na kupitisha Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, Miswada ya Sheria iliyojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017 (*The Railways Bill, 2017*), Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 3) wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments (No. 3) Bill, 2017*] na Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016. (*The Medical, Dental and Allied Health Professions Bill, 2016*).

Mheshimiwa Spika, maazimio yaliyowasilishwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu ni yafuatayo:-

(1) Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East African Community Protocol on Peace and Security*);

(2) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi*);

(3) Azimio la Bunge la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994; Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999; Itifaki Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004; Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008; na Itifaki Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani.

(4) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (*Intergovernmental Agreement – IGA*) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania).

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri iliyotolewa wakati wa kujadili Miswada na Maazimio hayo muhimu ambayo yana manufaa mengi kwa nchi yetu. Serikali itafanyia kazi maoni yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge lakini pia itachukua ushauri uliotolewa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri na umahiri mkubwa waliouonesha wakati wa kuwasilisha Miswada na Maazimio yaliyojadiliwa katika Mkutano huu pamoja na kutoa ufanuzi mbalimbali katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam wake kwa kazi kubwa na nzuri ya kuandaa Maazimio na Miswada iliyowasilishwa hapa Bungeni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2017/2018. Katika Mkutano wa Saba wa Bunge lako Tukufu, mwezi Juni, 2017 tulipitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2017/2018 ya jumla ya shilingi trilioni 31.7. Utekelezaji wa bajeti hiyo uliana mwezi Julai, 2017.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa bajeti hiyo na kwa ujumla mwenendo wa utekelezaji unaendelea kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka jitihada kubwa za kuimarisha ukusanyaji mapato ya ndani kwa kutumia mifumo ya kielektroniki. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai hadi Agosti, mwaka 2017, Serikali imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 2.448.

Mheshimiwa Spika, kati ya mapato hayo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya kiasi cha shilingi trilioni 2.305, sawa na asilimia 92 ya lengo la kukusanya jumla ya shilingi trilioni 2.492. Serikali inaendelea kuwahamasisha wafanyakishara kutumia mashine za kielektroniki za EFD katika kulipa kodi stahiki na kutoa ushirikiano kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kulipa kodi kwa hiari bila shuruti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya Serikali, katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Agosti, 2017, Serikali imetoa jumla ya shilingi trilioni 3.944 zinazotokana na mapato ya ndani na fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 3.107 ni fedha za matumizi ya kawaida ikijumuisha malipo ya mishahara ya Watumishi wa Umma na Deni la Taifa na Shilingi bilioni 836.8 zilitolewa na Hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika kipindi hicho cha miezi miwili, Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri zote nchini) zimepelekewa kiasi cha shilingi bilioni 117.558.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya fedha za matumizi ya maendeleo zilitolewa na Serikali kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Agosti, 2017 zinajumuisha kiasi cha shilingi bilioni 351.1 ambazo zimeelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kipaumbele na maeneo muhimu ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi ya kipaumbele iliyopewa fedha ni pamoja na miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara kuitia Mfuko wa Barabara (TANROADS na TARURA) shilingi bilioni 94.439; Mradi wa Nishati ya Umeme Vijiji (REA) shilingi bilioni 38.411; mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, shilingi bilioni 30.614; miradi ya maji kuitia Mfuko wa Maji , shilingi bilioni 20.740; na Mfuko wa Reli, shilingi bilioni 14.5.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni Mradi wa Ufuaji Umeme – Kinyerezi I – Extension - shilingi bilioni 14.702; ununuzi wa chakula cha Taifa kuitia NFRA, shilingi bilioni tano; mradi wa kujenga na kufufua maeneo ya viwanda kuitia SIDO, shilingi bilioni tano; mradi wa ununuzi na ukarabati wa meli za abiria na mizigo, shilingi bilioni 24.496; na shilingi bilioni 25 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi kwa ajili ya hospitali zetu. Tunaendelea na mradi wa kuimarisha Vituo vya Afya kwenye Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha zaidi za bajeti kwa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya kipaumbele kwa kadri tunavyoendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuendelea kuunga mkono na kushirikiana na Serikali katika jitihada hizi, hasa kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari na kutoa msukumo kwa Halmashauri kuweka nguvu zaidi katika kutumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya mfumo wa PLANREP na FFARS. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 5 Septemba, 2017, nikiwa hapa Dodoma nilipata fursa ya kuzindua mifumo miwili ya kielektroniki inayohusu kuboresha upangaji mipango na bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika ngazi za msingi zinazotoa elimu ya afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kwanza unahusu kuboresha taratibu za kupanga mipango, kuandaa bajeti na kutoa taarifa kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unaojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama “Planning, Budgeting and Reporting System - PlanRep”; na Mfumo wa Pili unahusu kuboresha taratibu za ukusanyaji mapato, malipo na kutoa taarifa za fedha za Vituo vya Umma vya kutolea huduma za Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; unaojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama “Facility for Financial Accounting and Reporting System - FFARS”.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, muda wote amekuwa akisisitiza kubana matumizi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali; na Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba kwa muda mrefu huko nyuma, tumekuwa tukitumia muda mrefu na gharama kubwa katika mchakato wa kuandaa na kuwasilisha Mipango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa; na za Mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vilevile, gharama kubwa zilitumika katika ufungaji wa Hesabu za Mwaka za Halmashauri na Mikoa. Uzinduzi wa mifumo hiyo miwili ya TEHAMA, unaenda sambamba na ndoto za Mheshimiwa Rais za kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kutumia vizuri rasilimali za umma. Napenda kueleza kwa kifupi manufaa na faida za Mifumo hii miwili ya malipo kwa kutoa taarifa ya fedha za vituo vya kutoa huduma, kuwa ni pamoja na:-

(i) Kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa Watumishi wa Umma hasa katika eneo la mapokezi ya fedha, utunzaji na matumizi ya fedha za umma. Hii ni kuanzia katika vituo vya kutolea huduma za elimu na afya vilivyopo vijijini hususan Vituo vya Afya, kama vile Zahaniati, vituo vya afya na hospitali yenyewe pia shule za msingi na sekondari hadi katika ngazi ya Halmashauri;

(ii) Kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi sahihi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia Mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano wa Serikali Kuu kupeleka fedha za matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za jamii ikiwemo elimu na afya;

(iii) Kupunguza na kuokoa wastani wa takriban Shilingi bilioni nne kila mwaka zilizokuwa zinatumika kwa ajili ya zoezi zima la kufanya maandalizi na mchakato wa kuandaa Mipango na Bajeti kuanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Taifa. Gharama hizo zilijumuisha kuandaa machapisho mbalimbali, nauli, mafuta pamoja na posho za kujikimu kwa Watumishi wanaoshiriki kuandaa Mipango na Bajeti za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa mifumo hii miwili, sasa ni wajibu wa kila Mkao, kila Halmashauri na Vituo vya kutolea huduma za elimu na afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa wadau husika na Mamlaka zinazohusika. Vilevile, ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa lazima zitoe taarifa za mapato na matumizi kwa wananchi wanaowahudumia kupitia mikutano, mbao za matangazo, tovuti zao, vyombo vya habari na njia nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali la kutumia mifumo ya TEHAMA ni kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za Serikali. Hivyo, ni muhimu mifumo hii iliyozinduliwa itumike kwa ufasaha ili kuleta tija inayotarajiwa na isitumike kukwamisha shughuli za Serikali au mipango ya utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kushirikiana na Serikali katika kufuatilia utekelezaji wa mifumo hii miwili ili ilete tija na ufanisi, hasa katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri; na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili fedha zilizotengwa zitumike ipasavyo; na ubora na thamani ya miradi inayotekelawa katika Halmashauri iwiiane na thamani ya fedha (yaani Value for Money); zilizotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuishukuru sana Serikali ya Marekani ambayo imetoa mchango mkubwa wa fedha katika kusaidia kuboresha mifumo hiyo miwili kupitia Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Sekta ya Umma (*Public Sector System Strengthening – PS3*). (Makofij)

Mheshimiwa Spika, aidha, kipekee niwashukuru Wataalam wetu wa ndani kutoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wataalam kutoka Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Watendaji wa ndani wa Mradi wa kuimarisha Mifumo ya Sekta ya Umma kwa kufanikiwa kutengeneza mifumo hii maalum ya kuandaa Mipango na Bajeti kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na ule wa usimamizi wa Fedha za Serikali katika ngazi za Msingi zinazotoa huduma za Elimu na Afya. Mifumo hii imebuniwa na Watanzania. Tunawashukuru sana na kuwapongeza sana Wataalam wetu Watanzania Wazalendo kwa ubunifu wao na umahiri waliouonesha katika kuboresha mifumo hii miwili.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa Sekta ya Madini; itakumbukwa kwamba yamekuwepo malalamiko kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, wananchi na Asasi mbalimbali wakionyesha kutoridhishwa kwao na mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa na usimamizi wa Serikali katika sekta hiyo. Aidha, yapo malalamiko kuwa Taifa letu limekuwa halinufaiki ipasavyo na sekta hii kwa sababu mikataba iliyopo haitoi fursa kwa Serikali kupata gawio la kutosha, kupata kodi na mapato mengine mbalimbali yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa madini zinazofanywa na makampuni yaliyopo nchini.

Mheshimiwa Spika, kupitia llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, ilitamka wazi kuwa itashughulikia kero ya umiliki wa rasilimali za nchi na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amesimamia vilivyo katika kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo. Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walijadili na kupitisha Miswada miwili ambayo ni Muswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi na pili ni Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mambo yaliyomo katika Miswada hiyo ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika umiliki wa rasilimali za nchi, uzuiaji wa usafirishaji wa rasilimali nje ya nchi kabla ya kuongezwa thamani, mashauri kati ya mwekezaji na Serikali kutopelekwa

Mahakama za nje na badala yake kutafutiwa ufumbuzi katika Mahakama za ndani pamoja na wawekezaji kuhifadhi fedha zao katika Benki za hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni pamoja na kadri inavyofaa kwa kulihusisha Bunge juu ya maslahi ya wananchi katika mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuza wao thabiti na wa kizalendo kwa kuzipitisha sheria hizi kwa manufaa ya Taifa na wananchi kwa ujumla. Serikali kwa upande wake imeanza utekelezaji wa usimamizi wa rasilimali hizi kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuunga mkono juhudzi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kuwa Watanzania na Taifa kwa ujumla wananaufaika ipasavyo na rasilimali za nchi yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo; jitihada zinazochukuliwa na Serikali kuimarisha uzalishaji wa mazao makuu ya biashara nchini. Naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kueleza kwa kifupi jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano na maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha usimamizi, uzalishaji na uuzaji wa mazao makuu matano ya awali ya biashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, maelekezo na jitihada hizi zina lengo la kuwawezesha wakulima wetu wengi wa vijiji ambao ni takriban asilimia 75 ya Watanzania wote, kulima kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibashara ili kuwawezesha kuondokana na umaskini. Vilevile, kuwawezesha wakulima kupata mbinu za kisasa za kuyafikia masoko ya uhakika ya mazao yao ili kupata bei nzuri na itakayowaongezea kipato chao.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeamua kuanza kwa kuweka mkazo wa kuyaendeleza kwa kasi mazao makuu matano ya biashara yakiwemo pamba, tumbaku, korosho, chai na kahawa. Mazao haya ni muhimu sana katika kuwawezesha mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kufikia uchumi wa viwanda. Mazao haya ndiyo mhimili wa kutoa malighafi za kuendesha viwanda husika na yana mnyororo mpana wa uzalishaji ambao una fursa ya kutoa ajira nyingi. Mazao mengine ya kibashara ambayo yatawekewa mkazo ni katani, ufuta, alizeti, mbaazi, ngano na kadhalika. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, pamoja na fursa kubwa tulio nayo ya kuendeleza mazao hayo, kwa kipindi kirefu uzalishaji wa mazao hayo makuu ya biashara ulishuka. Kushuka huko kulitokana na changamoto kadhaa zikiwemo kupungua tija katika uzalishaji, baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao hayo kutokana na wakulima kukatishwa tamaa na Viongozi wa Vyama vyao vya Ushirika kutotekeliza vyema wajibu wao, wizi, dhuluma kwa wakulima na pia ushiriki mdogo wa Maafisa Kilimo katika kusimamia Kilimo cha Kitaalam.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka kipaumbele cha kuzipatia ufumbuzi ili kuongeza uzalishaji na kukuza kipato cha mkulima.

Mheshimiwa Spika, moja ya hatua zinazochukuliwa na Serikali sasa ni kuyasimamia mazao hayo moja kwa moja kuptitia Maafisa Kilimo na Bodi za Mazao hayo. Serikali itahakikisha kuwa kila taasisi iliyopewa dhamana ya kusimamia mazao hayo, inatekeleza majukumu yake ipasavyo sambamba na kuhakikisha kwamba watendaji wake wa Serikali wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Vyama Vikuu na Vyama vya Msingi vya Mazao. Hivi karibuni Serikali imefanya uchunguzi ili kubaini changamoto zinazosababisha kupungua kwa uzalishaji wa

mazao haya matano ya biashara. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonesha kwamba, moja kati ya matatizo makubwa ni huduma zisizoridhisha za ugani na utafiti, ukosefu wa pembejeo bora, Vyama vingi vya Msingi na Vyama Vikuu vinachangia kuzorota kwa kilimo cha mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, Kwa muda mrefu Vyama vingi vya Ushirika vya mazao viligubikwa na ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa vyama hivyo na kusababisha kuyumba kwa bei kwenye soko la dunia. Bodi za Mazao kushindwa kusimamia kikamilifu uendelezaji wa mazao husika na badala yake wamewaachia wenye makampuni binafsi waendeleze mazao hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusimamia mazao hayo ziko jitihada zinaendelea za kuboresha mazao mengine ya kibiashara na chakula. Moja ya jitihada inayoendelea sasa ni kutafuta masoko ya mazao ambayo hayajanunuliwa kama vile tumbaku ipatayo tani zaidi ya 22,441 ambayo haijanunuliwa hadi sasa, mbaazi ambazo hazajanunuliwa na zimeshuka bei, chai ambayo ina migogoro katika Wilaya za Rungwe na Lushoto. Mazao haya yameshuka bei kutokana na kushuka kwa bei kwenye Soko la Dunia. Hata hivyo, Serikali inafanya jitihada za kutafuta masoko kwenye nchi hitaji, hivyo wakulima waendelee kuvuta subira.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja; Mazao ya Chakula; Serikali imeanza kutekeleza mfumo wa kuwawezesha wakulima kupata mbolea kwa gharama nafuu kwa kuagiza kwa pamoja kwa njia ya zabuni. Njia hii itashusha bei ya mbolea kutoka ya awali ya mfuko uliokuwa unauzwa kati ya Sh.70,000 - 100,000 na sasa utapatikana kwa bei ya chini kati ya Sh.53,000 - 60,000/=. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa kila mmoja atamudu kupata mbolea. Mbolea hizo zimeanza kuingia nchini tayari kwa kusambazwa na Serikali imeendelea kusimamia kuhakikisha mkulima ananufaika na mazao yake. Hata hivyo, Serikali imeweka mkazo ufuatao ili kukuza Sekta ya Kilimo:-

- (i) Maafisa Kilimo wa Wilaya, Maafisa Ugani wa Kata na Vijiji wasimamie kikamilifu mazao kutoka maandalizi ya mashamba hadi masoko yake;
- (ii) Kumfikishia mkulima pembejeo ikiwemo mbolea na mbegu kwa wakati;
- (iii) Kusimamia ushirika wa wakulima kama mazao hayo yana ushirika;
- (iv) Masoko ya mazao kwa kuondoa tozo zisizo na tija, mazao yote kununuliwa kwa fedha za Kitanzania, kwa mfano: zao la tumbaku kuanzia msimu ujao litanunuliwa kwa Fedha za Kitanzania badala ya Dola za Kimarekani; (Makofi)
- (v) Kupunguza vyombo/taasisi zinazosimamia mazao ili kuondoa mkanganyiko na urasimu wa utoaji huduma kwenye mazao hayo;
- (vi) Kusimamia mifumo ya masoko yake na kupambana na wanunuzi nje ya mifumo iliyokusudiwa. Mfano: Zao la korosho (kangomba) na zao la tumbaku (vishada). Mifumo hiyo kwa sasa haina nafasi tena kuanzia sasa.(Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Elimu, katika kipindi cha mwaka 2017/2018, Serikali imeendelea na mpango wa elimu bila malipo kwa kupeleka fedha moja kwa moja katika shule za umma za msingi na sekondari. Kiasi cha fedha kinachopelekwa shulenii kwa ajili ya kugharamia elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari ni jumla ya Shilingi bilioni 23.868 kwa mwezi. Kiwango hicho kimeongezeka kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa kwanza wa Sera ya Elimu bila Malipo ambapo kulikuwa na ongezeko kubwa la udahili wa

wanafunzi wa darasa la kwanza, kidato cha kwanza na cha tano pamoja na ongezeko la wanafunzi wa shule za umma za bweni.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kuhakikisha kuwa fedha za kugharamia elimu bila malipo zinatumika vizuri na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Waheshimiwa Wabunge mkiwa Viongozi na Madiwani kwenye Halmashauri zenu mnaombwa kuingilia kati na kuunga mkono Serikali kwa kufuatilia utekelezaji wa Sera hii hususan ufuatiliaji wa matumizi ya fedha hizo kwenye halmashauri zenu na kote nchini. Aidha, nawasihi wazazi kuendelea kuandikisha shule kila mtoto anayestahili kuijunga na elimu ya awali na darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Wanafunzi wa Kidato Cha Tano uliofanyika mwaka huu 2017. Katika Mwaka wa fedha wa 2017/2018, jumla ya wanafunzi 93,019 walikuwa na sifa za kujunga na kidato cha tano. Kati ya wanafunzi hao, Wanafunzi 71,987, sawa na asilimia 77.4 walichaguliwa katika Awamu ya kwanza na ya pili ili kuijunga na kidato cha tano mwaka huu. Majina ya wanafunzi waliobaki yamewasilishwa Baraza la Ufundsi la Taifa (National Council for Technical Education - NACTE) ili wapangiwe katika Vyuo vya Ufundsi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwafahamasisha wananchi kuendelea kujitolea kwa hali na mali kujenga shule za kidato cha tano na sita ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoijunga na vidato hivyo. Aidha, ni vema kipaumbele kiwekwe kwenye shule za bweni ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa usalama na kupata malezi bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuzifanya kazi changamoto zilizojitokeza katika upangaji wa wanafunzi kwenye shule za bweni. Kama ilivyodokezwa na Waheshimiwa Wabunge katika michango mbalimbali hapa Bungeni. Lengo ni kuhakikisha nafasi zilizopo katika shule zote za bweni zinatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya, Upatikanaji wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendenishi. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendenishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeendelea kuimarika, ambapo kwa mwezi Julai na Agosti 2017, kiwango cha upatikanaji wa dawa katika Bohari ya Dawa kimeongezeka hadi kufikia asilimia 82 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 50 kwa kipindi cha mwaka 2016/2017. Aidha, kiwango cha upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya kimeongezeka hadi kufikia asilimia 90 kutoka asilimia 60 katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yanatokana na Serikali kuongeza mgao wa fedha katika Sekta ya Afya nchini kutoka Shilingi trilioni 1.988 mwaka 2016/2017 hadi kufikia Shilingi trilioni 2.222 kwa mwaka 2017/2018. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 11.77. Aidha, bajeti ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendenishi imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/2016 hadi kufikia Shilingi bilioni 269 mwaka wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya pia yametokana na Bohari ya Dawa kuanza kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendenishi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji badala ya washitiri wa kati waliokuwa wanauzu bidhaa hizo kwa gherama kubwa. (Makofij)

Vituo vya kutolea huduma za afya kuwa na vifaa vya kutosha ni mkakati ambao kwa sasa unaendelea ndani ya Serikali. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliahidi kuwa, Serikali itahakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya nchini kinakuwa na vifaa vya kutosha, kutakuwa na dawa ili kuwawezesha watoa huduma kutoa huduma bora kwa wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ahadi hii ulianza mwezi Aprili 2017, ambapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilianza kusambaza vitanda ishirini vya kawaida, vitanda vitano vya kujifungulia, magodoro ishirini na tano na mashuka hamsini katika vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Agosti 2017; Serikali imekamilisha kusambaza vifaa vifuatavyo: jumla ya vitanda 3,208 katika Halmashauri 162; magodoro 3,189 katika Halmashauri 160; mashuka 7,570 katika Halmashauri 159; na jumla ya vitanda 322 vya kujifungulia, katika Halmashauri 69 nchini. (Makof)

Mheshimiwa Spika, usambazaji wa vifaa hivyo umekamilika kwa asilimia 85. Serikali inaendelea na zoezi la usambazaji wa vifaa hivyo na kukamilisha kazi hii katika kipindi kifupi iwezekanavyo ili kuwawezesha wananchi kupata huduma bora za afya pindi wanapozihitaji. Jambo la msingi kwa Watendaji katika ngazi mbalimbali ni kuhakikisha katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali na akinamama wajawazito wanapata matibabu bure. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Uwezesajji Vijana; kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 asilimia zaidi ya 35 ya Watanzania ni vijana na hivyo, Serikali imeamua kuandaa mpango wa kuwekeza kwao ili nguvu kazi hii iweze kuchangia kikamilifu katika kujenga uchumi wa Taifa kuititia Mpango wa Kutathmini na Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo. Jumla ya Vijana 1,000 wamelengwa kupata urasimishaji ujuzi kati ya mwaka 2017 na 2021. Hadi sasa vijana kadhaa wanaendelea kunufaika na mpango huu kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa faida za program hii ni pamoja na: Kuwasaidia mafundi waliojifunza kuititia sehemu za kazi, kupata kazi zenyenye staha na kuwajengea uwezo wa kushiriki katika kushindana kikamilifu katika soko la ajira, lakini pia kuinua tija mahali pa kazi na kusaidia waajiri wenye makampuni kukidhi viwango katika eneo la rasili mali watu. Mpango huu unafadhiliwa kwa asilimia mia moja na Serikali yetu na unatekelezwa kwa pamoja na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Barabara; Kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (TARURA), Tanzania Rural and Urban Road Agency. Sote tunatambua kilio kikubwa na cha muda mrefu kilichotolewa na wadau mbalimbali wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwemo Waheshimiwa Madiwani na sisi pia Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wananchi na Wadau wa Sekta ya Barabara kuhusu umuhimu wa kuwa na Wakala wa Barabara Vijiji. Aidha, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015, katika Ibara ya 39(a)(3), Ukurasa wa 54, inaielekeza Serikali kuanzisha mamlaka au taasisi itakayosimamia kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara za halmashauri mijini na vijiji, kwenye majiji ambazo ziko chini ya TAMISEMI ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, tayari Serikali imeunda Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini unaojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama, Tanzania Rural and Urban Road Agency (TARURA). Siku ya tarehe 2 Julai, 2017, nilipata nafasi ya kuzindua rasmi wakala huo hapa Mjini Dodoma. Wakala huo umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura Namba 245 na ultangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali Namba 211 la tarehe 12 Mei, 2017.

Mheshimiwa Spika, TARURA imeanzishwa rasmi ikiwa ni jitihada za Serikali za kuimarisha sekta ya barabara za mijini na vijiji. Aidha, uzinduzi wa Wakala huu ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kuboresha maisha ya wananchi, hususan waishio vijiji na kuwawezesha kusafiri na kuendesha shughuli za kibashara kwa urahisi. Majukumu ya Wakala ni ujenzi, ukarabati na matengenezo ya madaraja ya barabara za vijiji na mijini

zilizokuwa zikitengenezwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili kuimarisha usafirishaji na usafirishaji wa mazao wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji kunatarajia kuondoa kero zifuatazo:-

(i) Barabara za halmashauri kujengwa chini ya kiwango tena kwa kutumia muda mrefu kuliko makubaliano ya kimkataba;

(ii) Tabia ya baadhi ya viongozi na watendaji wasio waadilifu wanaoziibia halmashauri kupitia kandarasi za ujenzi wa barabara; na

(iii) Kuondoa migongano ya kimaslahi mionganoni mwa baadhi ya Madiwani na Watumishi wa Halmashauri katika kusimamia ujenzi wa barabara za halmashauri kupitia zabuni zinazosimamiwa na halmashauri.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa TARURA itasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha mitandao ya barabara ya vijiji na hivyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kusafiri na kusafirisha bidhaa za mashambani kwa urahisi, ndio kichocheo cha ukuaji wa uchumi vijiji. Naomba kutoa rai kwa wadau wote wa barabara nchini, wakiwemo Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na sisi Waheshimiwa Wabunge tukiwemo na Waheshimiwa Madiwani kuusoma vizuri mpango kazi wa Wakala huo ili kutoa msukumo katika kuboresha barabara za vijiji na mijini zilizopo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imepokea hoja ya Waheshimiwa Wabunge ya kupewa ufanuzi wa kutosha kuhusu majukumu ya TARURA. Hoja hiyo itafanyiwa kazi mapema iwezekanavyo ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani na Wadau wote kuilewa vizuri, lakini pia kuisimamia na kuisimamia vizuri Serikali kwenye maeneo haya inapotekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuwashukuru tena wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu wa Bunge. Shukrani za pekee ni kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao pamoja na Watumishi wote wa Serikali waliosaidia Serikali kujibu maswali na kuwasilisha hoja za Serikali hapa Bungeni. (Makof)

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wenyeiti wa Bunge ambaa pia nao wameshirikiana nawe katika kuliongoza Bunge hili. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kipekee, namshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha Mkutano huu. Nawashukuru wale wote waliokuwa na jukumu la ulinzi na usalama ili kuhakikisha kwamba, Mkutano huu unafanyika na kumalizika salama. (Makof)

Mheshimiwa Spika, napenda pia, niwashukuru madereva wote kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa kwa kuwaleta Waheshimiwa Wabunge na sasa tukiwa tunarudi nawatakia safari njema zenyeheri na baraka huko mwendako. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Waandishi wa Habari kwamba, tumeshirkiana kwa pamoja na kuhakikisha kuwa habari za hapa Bungeni zinawafikia wananchi katika namna mbalimbali. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Dodoma na wa Mji wa Dodoma kwa ukarimu wao kwa kutupatia huduma zote muhimu na kuishi hapa kwa usalama na hivyo, kukamilisha Mkutano huu leo kwa mafanikio makubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu, sasa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 7 Novemba, 2017 litakapokutana tena hapa, Saa tatu asubuhi, hapa Mjini Dodoma. (Makofii)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yako nzuri, makini iliyotufikisha hapa. Tunasema asante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba hiyo yenyе umakini mkubwa sana. (Makofii)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA NANE WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, TAREHE 15 SEPTEMBER, 2017 – DODOMA KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 5 Septemba, 2017 tulianza Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Nane wa Bunge lako Tukufu na leo tunafikia tamati. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwa amani, salama, tukiwa na afya na uzima.
2. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kutumia nafasi hii ya awali kukupongeza Mheshimiwa Spika, kwa hekima, busara na uwezo mkubwa wa kuliongoza Bunge hili ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Waheshimiwa Wabunge watakulaliana nami kwamba kwa mara nyingine ushuhuda huu ni dhahiri na umejidhihirisha wazi katika kikao hiki ambapo mmeongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuendelea kuonesha ukomavu wa Kisiasa kwa kuwa wavumilivu sana. Vilevile, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi nzuri pamoja na michango yenu mizuri ya maoni na ushauri tuliuopokea wakati wa mijadala ya Hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu.
3. **Mheshimiwa Spika**, wakati tukiendelea na kikao hiki cha Bunge, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge na Wananchi tunaowawakilisha katika Majimbo yetu walipata Misiba ya Ndugu, Jamaa na Marafiki. Nitumie nafasi hii kuwapa pole wote waliofikwa na Misiba hiyo. Aidha, kama ambavyo wote tunakumbuka mnamo tarehe 7 Septemba, 2017 tulipata taarifa ya tukio la kusikitisha lililotokea hapa Dodoma la mashambulizi na kupigwa risasi kwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Tundu Antipas Lissu (Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki) Naungana na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge pamoja na Wananchi mbalimbali kwa kumpa pole kwa majeraha na maumivu makubwa aliyo yapata, tunamwombea apone haraka na kurejea kuungana na familia yake, pia nasi kwa shughuli za hapa Bungeni.
4. **Mheshimiwa Spika**, Nitumie nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoa pole nyingi kwa Meja Jenerali Mstaafu Vicent Mritaba kutokana na tukio la kushambuliwa kwa risasi siku ya Jumatatu tarehe 11 Septemba, 2017 nyumbani kwake ambaye bado anaendelea na matibabu kwenye Hosptitali ya Lugalo.

Serikali inalaani vitendo hivyo na matukio hayo ya kinyama. Ni mwezi na nusu sasa tumeanza kuanza utulivu kufuatia vifo vya Raia na Askari wetu wa Jeshi la Polisi waliouawa kikatili huko maeneo ya Mbagala - Dar es Salaam, Mkuranga, Rufiji na Kibiti, Mkoa wa Pwani. Nitumie fursa hii kusisitiza kwamba kwa matukio haya Serikali haitafumbia macho na tayari Vyombo vya Dola vimeagizwa kuhakikisha kwamba vinawatafuta kwa mbinu zote wale wote waliohusika katika vitendo hivyo. Nirejee kuwasihii Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wavute subira wakati Serikali na Vyombo vya Dola vinashughulikia matukio haya kwa umakini mkubwa. Jambo la msingi ni kwamba kila mmoja wetu adumishe hali ya ulinzi na usalama Nchini.

### PONGEZA KWA WABUNGE WAPYA

5. **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu liliwaapisha Waheshimiwa **Wabunge Wapya Nane** wa Viti Maalum walioteuliwa hivi karibuni. Napenda kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote hao, amba ni Mhe. Alfredina Apolinary Kahigi (Mb.); Mhe. Kiza Hussein Mayeye (Mb.); Mhe. Nuru Awadh Bafadhili (Mb.); Mhe. Rukia Ahmed Awadh (Mb.); Mhe. Shamsia Aziz Mtamba (Mb.); Mhe. Sonia Jumaa Magogo (Mb.); Mhe. Zainab Mndolwa Amir (Mb.); na Mhe. Rehema Juma Migila (Mb.).

### PONGEZA KWA JAJI MKUU WA TANZANIA

6. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 10 Septemba, 2017 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alimteua Mheshimiwa Jaji Profesa Ibrahim Hamis Juma kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania. Napenda kupitia Bunge lako tukufu nimpongeze Mheshimiwa Profesa Ibrahim Hamis Juma kwa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania. Serikali ya Awamu ya Tano itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwake katika kuongoza Muhimili wa Mahakama. Aidha, nampongeza Jaji Mkuu Mstaafu Chande Othman kwa kazi kubwa na nzuri aliyofanya katika kipindi chake cha Uongozi wa Muhimili huo, hususan kuweka misingi imara ya Muhimili wa Mahakama.

### MASWALI, MISWADA NA MAAZIMIO

7. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya kawaida ya msingi yapatayo **119** na maswali **295** ya nyongeza na kujibiwa na Serikali. Vilevile, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili Miswada Mitatu na Maazimio Manne. Vilevile, Bunge lako Tukufu lilipokea na kupitisha taarifa ya Kamati ya Sheria ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge.

8. **Mheshimiwa Spika**, Miswada ya Sheria iliyojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu ni:

(i) Muswada wa Sheria ya Reli wa Mwaka 2017 (*The Railways Bill, 2017*);

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2017 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments - No.3), Bill, 2017*];

(iii) Muswada wa Sheria ya Madaktari, Madaktari wa Meno na Wataalam wa Afya Shirikishi wa Mwaka 2016. (*The Medical, Dental and Allied Health Professions Bill, 2016*).

9. **Mheshimiwa Spika**, Maazimio yaliyowasilishwa na kuridhiwa na Bunge lako Tukufu ni yafuatayo:

(i) Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; (*East African Community Protocol on Peace and Security*);

(ii) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Kamisheni ya pamoja ya Bonde la Mto Songwe kati ya Tanzania na Malawi (*Convention on the Establishment of a Joint Songwe River Basin Commission Between Tanzania and Malawi*);

(iii) Azimio la Bunge la Bunge la Kuridhia Itifaki Nyongeza ya Tano ya Mwaka 1994; Itifaki Nyongeza ya Sita ya Mwaka 1999; Itifaki Nyongeza ya Saba ya Mwaka 2004; Itifaki Nyongeza ya Nane ya Mwaka 2008; na Itifaki Nyongeza ya Tisa ya Mwaka 2016 ya Katiba ya Umoja wa Posta Duniani;

(iv) Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba (*Intergovernmental Agreement – IGA*) baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uganda kuhusu Mradi wa Ujenzi wa bomba la kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (*East Africa Crude Oil Pipeline – EACOP*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania);

10. **Mheshimiwa Spika**, napenda kurejea tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri iliyotolewa wakati wa kujadili Miswada na Maazimio hayo muhimu ambayo yana manufaa mengi kwa Nchi yetu. Serikali itafanya kazi maoni na ushauri uliotolewa

11. **Mheshimiwa Spika**. Napenda kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri na umahiri mkubwa waliounesha wakati wa kuwasilisha Miswada na Maazimio yaliyojadiliwa katika Mkutano huu pamoja na kutoa ufanuzi mbalimbali katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalam wake kwa kazi kubwa na nzuri ya kuandaa kwa wakati Maazimio na Miswada iliyowasilishwa hapa Bungeni.

#### **MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI 2017/2018**

12. **Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Saba wa Bunge lako Tukufu, mwezi Juni, 2017 tulipitisha Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2017/2018 ya jumla ya Shilingi **Triliioni 31.7**. Utekelezaji wa Bajeti hiyo ulianza Mwezi Julai, 2017. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Bajeti hiyo na kwa ujumla mwenendo wa utekelezaji unaridhisha.

13. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeweka jitihada kubwa za kuimarisha ukusanyaji mapato ya ndani kwa kutumia mifumo ya kielektroniki. Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai hadi Agosti, 2017, Serikali imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **Triliioni 2.448**. Kati ya mapato hayo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekusanya kiasi cha Shilingi **Triliioni 2.305**, sawa na **Asilimia 92** ya lengo la kukusanya jumla ya Shilingi **Triliioni 2.492**. Serikali inaendelea kuwahamasisha Wafanyabiashara kutumia mashine za kielektroniki za EFD katika kulipa kodi stahili na kutoa ushirikiano kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kulipa kodi kwa hiari bila shuruti.

14. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya Serikali, katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Agosti, 2017 Serikali imetua jumla ya Shilingi **Triliioni 3.944** zinazotokana na mapato ya ndani na fedha za nje. Kati ya fedha hizo, Shilingi **Triliioni 3.107** ni Fedha za Matumizi ya Kawaida ikijumuisha malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma na Deni la Taifa na Shilingi **Bilioni 836.8** zilitolewa na HAZINA kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika kipindi hicho cha miezi miwili, **Mamlaka za Serikali za Mitaa** (Halmashauri zote Nchini) zimepelekewa kiasi cha Shilingi **Bilioni 117.558**.

15. **Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Fedha za Matumizi ya Maendeleo zilizotolewa na Serikali kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Agosti, 2017 zinajumuisha kiasi cha Shilingi **Bilioni 351.1** ambazo zimeelekezwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kipaumbele na maeneo muhimu

ya huduma za Jamii. Baadhi ya miradi ya kipaumbele iliyopewa fedha ni pamoja na Miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara kupitia Mfuko wa Barabara (TANROADS na TARURA) - Shilingi **Bilioni 94.439**; Mradi wa Nishati ya Umeme Vijijini (REA) - Shilingi **Bilioni 38.411**; Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu - Shilingi **Bilioni 30.614**, Miradi ya Maji kupitia Mfuko wa Maji - Shilingi **Bilioni 20.740** na Mfuko wa Reli - Shilingi **Bilioni 14.5**. Maeneo mengine ni Mradi wa ufuaji umeme – Kinyerezi I – Extension - Shilingi **Bilioni 14.702**; Ununuzi wa Chakula cha Taifa kupitia NFRA - Shilingi **Bilioni 5**; Mradi wa kujenga na kufufua maeneo ya Viwanda kupitia SIDO - Shilingi **Bilioni 5**, Mradi wa ununuzi na ukarabati wa meli za abiria na mizigo, Shilingi **Bilioni 24.496; na Shilingi Bilioni 25** kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi. Tunaendelea na mradi wa kuimarisha Vituo vya Afya.

16. **Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kutoa fedha zaidi za Bajeti kwa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya kipaumbele kwa kadri tunavyoendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuendelea kuunga mkono na kushirikiana na Serikali katika jitihada hizi, hasa kuhamasisha Wananchi kulipa kodi kwa hiari na kutoa msukumo kwa Halmashauri kuweka nguvu zaidi katika kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa Mapato.

#### **MABORESHO YA MFUMO WA PLANREP NA FFARS**

17. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba tarehe 5 Septemba, 2017 nikiwa hapa Dodoma nilipata fursa ya kuzindua mifumo **miwili** ya kielektroniki inayohusu kuboresha Upangaji Mipango na Bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na kuimarisha usimamizi wa fedha za Umma katika ngazi za msingi zinazotoa huduma za Elimu na Afya. **Mfumo wa Kwanza** unahusu kuboresha taratibu za kupanga Mipango, kuandaa Bajeti na kutoa Taarifa kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unaojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama “*Planning, Budgeting and Reporting System - PlanRep*”; na **Mfumo wa Pili** unahusu kuboresha taratibu za ukusanyaji mapato, malipo na kutoa taarifa za fedha za Vituo vya Umma vya kutolea huduma za Jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; unaojulikana kwa lugha ya Kiingereza kama “*Facility for Financial Accounting and Reporting System - FFARS*”.

18. **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania muda wote amekuwa akisisitiza kubana matumizi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali; na Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba kwa muda mrefu huko nyuma, tumekuwa tukitumia muda mrefu na gharama kubwa katika mchakato wa kuandaa na kuwasilisha Mipango na Bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa; na za Mamlaka mbalimbali za Serikali. Vilevile, gharama kubwa zilitumika katika ufungaji wa Hesabu za Mwaka za Halmashauri na Mikoa. Uzinduzi wa mifumo hiyo miwili ya TEHAMA, unaenda sambamba na azma ya Mheshimiwa Rais ya kuhimiza kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kutumia vizuri rasilimali za umma. Napenda kueleza kwa kifupi manufaa na faida za Mifumo hiyo ya “*PLANREP*” na Mfumo wa malipo na kutoa taarifa za fedha za vituo vya kutolea huduma, kuwa ni pamoja na:-

**Moja:** Kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa Watumishi wa Umma hasa katika eneo la mapokezi ya fedha, utunzaji na matumizi ya Fedha za Umma. Hii ni kuanzia katika vituo vya kutolea huduma za Elimu na Afya vilivyopo Vijijini (hususan Vituo vya Afya, Zahanati na Shule za Msingi na Sekondari) hadi katika ngazi ya Halmashauri;

**Mbili:** Kuimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi sahihi ya fedha za Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia Mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano wa Serikali Kuu kipeleka Fedha za matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo moja kwa moja katika vituo vya kutolea huduma za Jamii ikiwemo Elimu na Afya;

**Tatu:** Kupunguza na kuokoa wastani wa takriban Shilingi **Bilioni 4** kila mwaka zilizokuwa zinatumika kwa ajili ya zoezi zima la kufanya maandalizi na mchakato wa kuanda Mipango na Bajeti kuanzia ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hadi Taifa. Gharama hizo zilijumuisha kuanda machapisho mbalimbali, nauli, mafuta pamoja na posho za kujikimu kwa Watumishi wanaoshiriki kuanda Mipango na Bajeti za Halmashauri.

19. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kukamilika kwa mifumo hii miwili, sasa ni wajibu wa kila Mkoa, kila Halmashauri na Vituo vya kutolea huduma za Elimu na Afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa taarifa ya mapato na matumizi kwa Wadau husika na Mamlaka zinazohusika. Vilevile, **ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa lazima zitoe taarifa za mapato na matumizi kwa Wananchi wanaowahudumia kupitia mikutano, mbao za matangazo, tovuti zao, vyombo vya habari** na njia nyinginezo;

20. **Mheshimiwa Spika**, lengo la Serikali la kutumia mifumo ya TEHAMA ni kuongeza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika utendaji kazi wa shughuli za Serikali. Hivyo, ni muhimu mifumo iliyozinduliwa itumike kwa ufasaha ili kuleta tija inayotarajiwa na isitumike kukwamisha shughuli za Serikali au mipango ya utoaji huduma kwa wananchi.

21. **Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kushirikiana na Serikali katika kufuatilia utekelezaji wa Mifumo hii miwili ili ilete tija na ufanisi, hasa katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri; na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili fedha zilizotengwa zitumike ipasavyo; na ubora na thamani ya miradi inayotekelawa katika Halmashauri iwiante na thamani ya fedha (yaani Value for Money); zilizotolewa na Serikali.

22. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Serikali ya Marekani ambayo imetoa mchango mkubwa wa fedha katika kusaidia kuboresha mifumo hiyo miwili kupitia Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Sekta ya Umma (*Public Sector System Strengthening – PS3*). Aidha, kipekee niwashukuru Wataalam wetu wa ndani kutoka Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Wataalam kutoka Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na Watendaji wa ndani wa Mradi wa kuimarisha Mifumo ya Sekta ya Umma (PS3); kwa kufanikiwa kutengeneza mifumo hii maalum ya kuanda Mipango na Bajeti kwa ajili ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na ule wa usimamizi wa Fedha za Serikali katika ngazi za Msingi zinazotoa huduma za Elimu na Afya. Mifumo hii imebuniwa na Watanzania. Tunawashukuru na kuwapongeza sana Wataalam wetu Watanzania Wazalendo kwa ubunifu wao na umahiri walionunesha katika kuboresha Mifumo hii miwili.

## USIMAMIZI WA SEKTA YA MADINI

23. **Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba yamekuwepo malalamiko kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, Wananchi na Asasi mbalimbali wakionesha kutoridhishwa kwao na mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa na usimamizi wa Serikali katika Sekta hiyo. Aidha, yapo malalamiko kuwa Taifa letu limekuwa halinufaiki ipasavyo na Sekta hii kwa sababu mikataba iliyopo haitoi fursa kwa Serikali kupata gawio la kutosha, kupata kodi na mapato mengine mbalimbali yanayotokana na shughuli za uchimbaji wa madini zinazofanywa na makampuni yaliyopo nchini.

24. **Mheshimiwa Spika**, Kupitia llani ya Uchaguzi wa CCM ya Mwaka 2015 ilitamka wazi kuwa itashughulikia kelo ya umiliki wa rasilimali za Nchi na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amesimamia vilivyo. Katika kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walijadili na kupitisha Miswada miwili ambayo ni Miswada wa Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu masharti hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi, na pili ni Miswada wa Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya Mwaka 2017.

25. **Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa mambo yaliyomo katika miswada hiyo ni pamoja na ushirikishwaji wa wananchi katika umiliki wa rasilimali za Nchi, uzuiaji wa usafirishaji wa rasilimali nje ya nchi kabla ya kuongezwa thamani, mashauri kati ya mwekezaji na Serikali kutopelekwa Mahakama za Nje na badala yake kutafutiwa ufumbuzi katika Mahakama za Ndani pamoja na wawekezaji kuhifadhi fedha zao katika Benki za hapa nchini. Jambo jingine ni pamoja na kadri inavyofaa kwa kulihusisha Bunge juu ya maslahi ya Wananchi katika Mikataba hii.

26. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuza wao thabit na wa kizalendo kwa kuzipitisha sheria hizi kwa manufaa ya Taifa na Wananchi kwa ujumla. Serikali kwa upande wake imeanza utekelezaji wa usimamizi wa rasilimali hizi kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

Aidha, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Watanzania kuunga mkono juhud za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuhakikisha kuwa Watanzania na Taifa kwa ujumla wananaufaika ipasavyo na rasilimali za Nchi yao.

## SEKTA YA KILIMO

### JITIHADA ZINAZOCHUKULIWA NA SERIKALI KUIMARISHA UZALISHAJI WA MAZAO MAKUU MATANO YA BIASHARA NCHINI

27. **Mheshimiwa Spika**, naomba uniruhusu nitumie nafasi hii kueleza kwa kifupi jitihada za Serikali ya awamu ya Tano na maelekezo mahsus ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuimarisha usimamizi katika uzalishaji na uuzaji wa mazao makuu matano ya awali ya biashara hapa Nchini. Maelekezo na jitihada hizi zina lengo la kuwawezesha Wakulima wetu wengi wa Vijiini ambao ni takriban **Asilimia 75** ya Watanzania wote, kulima **kilimo cha kisasa, chenye tija na cha kibiashara** ili kuwawezesha kuondokana na umaskini. Vilevile, kuwawezesha wakulima kupata mbinu za kisasa za kuyafikia masoko ya uhakika ya mazao yao ili kupata bei nzuri na itakayowaongezea kipato.

28. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza azma hiyo, Serikali imeamua kuanza kwa kuweka mkazo wa kuyaendeleza kwa kasi mazao makuu matano ya biashara yakiwemo **Pamba, Tumbaku, Korosho, Chai na Kahawa**. Mazao haya ni muhimu sana katika kuwezesha mkakati wa Serikali ya awamu ya Tano wa kufikia uchumi wa viwanda. Mazao haya ndiyo mhimili wa kutoa malighafi za kuendesha viwanda husika na yana mnyororo mpana wa uzalishaji ambao una fursa ya kutoa ajira nydingi. Mazao mengine ya Kibiashara ambayo yatawekewa mkazo ni **Katani, Ufuta, Alizeti, Mbazi, Ngano** n.k.

29. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na fursa kubwa tuliyo nayo ya kuendeleza mazao haya, kwa kipindi kirefu uzalishaji wa mazao haya makuu ya biashara ulishuka. Kushuka huko kulitokana na changamoto kadhaa zikiwemo kupungua tija katika uzalishaji, baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao haya kutookana na Wakulima kukatishwa tamaa na Viongozi wa Vyama vyao vya ushirika kutotekeliza vyema wajibu wake Wizi, dhuluma kwa Wakulima na pia ushiriki mdogo wa Maafisa Kilimo katika kusimamia Kilimo cha Kitaalam.

30. **Mheshimiwa Spika**, ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali ya Awamu ya Tano imeweka kipaumbele cha kuzipatia ufumbuzi ili kuongeza uzalishaji na kukuza kipato cha mkulima. Moja ya hatua zinazochukuliwa na Serikali ni kuyasimamia mazao haya moja kwa moja kupitia Maafisa Kilimo na Bodi za Mazao haya. Serikali itahakikisha kuwa kila taasisi iliyopewa dhamana ya kusimamia mazao haya, inatekeleza majukumu yake ipasavyo sambamba na kuhakikisha kwamba Watendaji wake wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu na ufanisi mkubwa.

## VYAMA VIKUU NA VYAMA VYA MSINGI VYA MAZAO

31. **Mheshimiwa Spika**, hivi karibuni Serikali imefanya uchunguzi ili kubaini changamoto zinazosababisha kupungua kwa uzalishaji wa mazao haya matano ya biashara. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonesha kwamba, huduma zisizoridhisha za ugani na utafiti. Ukosefu wa Pembejeo bora, Vyama vingi vya Msingi na Vyama Vikuu vinachangia kuzorota kwa kilimo cha mazao hayo. Kwa muda mrefu vyama vingi vya ushirika wa mazao viligubikwa na ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya Viongozi wa Vyama hivyo.

- Kuyumba kwa bei kwene soko la dunia.
- Bodi za Mazao kushindwa kusimamia kikamilifu uendelezaji wa mazao husika na badala yake wamewaachia wenyе makampuni binafsi waendeleze mazao hayo;

32. **Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kusimamia Mazao hayo ziko jitihada zinaendelea za kuboresha Mazao mengine ya kibiashara na chakula. Moja ya jitihada inayoendelea sasa ni kutafuta Masoko ya Mazao ambayo hayajanunuliwa kama vile **Tumbaku** ipatayo **Tani zaidi ya 22,441** ambayo haijanunuliwa hadi sasa, Mbaazi ambazo hazijanunuliwa na zimeshuka bei, Chai ambayo ina migogoro katika Wilaya za Rungwe na Lushoto. Mazao haya yameshuka bei kutokana na kushuka kwa bei kwene Soko la Dunia. Hata hivyo Serikali inafanya jitihada za kutafuta Masoko kwenye Nchi hitaji. Hivyo Wakulima wavute subira.

## MFUMO WA UNUNUZI WA MBOLEA KWA PAMOJA

33. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeanza kutekeleza mfumo wa kuwawezesha Wakulima kupata Mbolea kwa gharama nafuu kwa kuagiza kwa pamoja kwa njia ya zabuni. Njia hii itashusha bei kutoka ya awali ya Mfuko uliokuwa unauzwa kati ya Tsh. **70,000 - 100,000** na sasa utapatikana kwa kati ya Tsh. **53,000 - 60,000/=**.

34. **Mheshimiwa Spika**, Ni matumaini yetu kuwa kila mmoja atamudu kupata Mbolea. Mbolea hizo zimeanza kuingia nchini tayari kwa kusambazwa na Serikali imeendelea kusimamia kuhakikisha mkulima ananufaika na mazao yake. Hata hivyo, Serikali imeweka mkazo ufuatao ili kukuza Sekta ya Kilimo:-

- (i) Maafisa Kilimo (W), Maafisa Ugani Kata na Vijiji kusimamia mazao katika maandalizi ya mashamba - masoko.
- (ii) Kumfikishia mkulima Pembejeo ikiwemo mbolea na mbegu kwa wakati.
- (iii) Kusimamia ushirika wa wakulima.
- (iv) Masoko ya mazao kwa kuondoa tozo zisizo na tija, mazao yote kununuliwa kwa fedha za Kitanzania, kwa mfano: zao la Tumbaku kuanzia msimu ujao litanunuliwa kwa Fedha za Kitanzania badala ya Dola za Kimarekani.
- (v) Kupunguza Vyombo/Taasisi zinazosimamia mazao ili kuondoa mkanganyiko wa utoaji huduma.
- (vi) Kusimamia mifumo ya masoko yake na kupambana na wanunuzi nje ya mifumo iliyokusudiwa. Mfano: Zao la Korosho (Kangomba) na zao la Tumbaku (Vishada). Mifumo hiyo kwa sasa haina nafasi.

## SEKTA YA ELIMU

35. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2017/2018 Serikali imeendelea na mpango wa Elimu bila malipo kwa kupeleka fedha moja kwa moja katika Shule za Umma za Msingi na Sekondari. Kiasi cha fedha kinachopelekwa shulenii kwa ajili ya kugharamia elimu bila malipo kwa Shule za Msingi na Sekondari ni jumla ya Shilingi **Bilioni 23.868** kwa mwezi. Kiwango hicho kimeongezeka kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa kwanza wa sera ya elimu bila malipo ambapo kulikuwa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi wa darasa la Kwanza, Kidato cha kwanza na cha tano pamoja na ongezeko la wanafunzi wa shule za umma za bweni.

36. **Mheshimiwa Spika**, natoa wito kwa Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kuhakikisha kuwa fedha za kugharamia elimu bila malipo zinatumika vizuri na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Waheshimiwa Wabunge mkiwa Viongozi na Madiwani kwenye Halmashauri zenu mnaombwa kuiunga mkono Serikali kwa kufuatilia utekelezaji wa Sera hii hususan ufuatiliaji wa matumizi ya fedha hizo kwenye Halmashauri zenu na kote nchini. Aidha, nawasihi wazazi kuendelea kuandikisha shule kila mtoto anayestahili kujunga na elimu ya awali na darasa la kwanza.

## UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO MWAKA 2017/2018

37. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa fedha wa 2017/2018 jumla ya wanafunzi **93,019** walikuwa na sifa za kujunga na kidato cha Tano. Kati ya wanafunzi hao, Wanafunzi **71,987**, sawa na **Asilimia 77.4** walichaguliwa katika Awamu ya kwanza na ya pili ili kujunga na kidato cha Tano mwaka huu. Majina ya wanafunzi waliobaki yamewasilishwa Baraza la Ufundsi la Taifa (**National Council for Technical Education - NACTE**) ili wapangiwe katika Vyuo vya Ufundsi.

38. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashamasisha wananchi kuendelea kujitolea kwa hali na mali kujenga shule za kidato cha tano na sita ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vidato hivyo. Aidha, ni vema kipaumbele kiwekwe kwenye shule za bweni ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza kwa usalama na kupata malezi bora. Serikali inaendelea kuzifanyia kazi changamoto zilizojitokeza katika upangaji wa Wanafunzi kwenye Shule za bweni. Kama ilivyodokezwa na Waheshimiwa Wabunge katika michango mbalimbali hapa Bungeni. Lengo ni kuhakikisha nafasi zilizopo katika Shule zote za bweni zinatumika ipasavyo.

## SEKTA YA AFYA

### UPATIKANAJI WA DAWA, VIFAA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

39. **Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeendelea kuimarika, ambapo, kwa mwezi Julai na Agosti 2017, kiwango cha upatikanaji wa dawa katika Bohari ya Dawa kimeongezeka hadi kufikia asilimia **82** ikilinganishwa na wastani wa asilimia **50** kwa kipindi cha Mwaka 2016/17. Aidha, kiwango cha upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya kimeongezeka hadi kufikia asilimia **90** kutoka asilimia **60** katika Mwaka wa fedha 2016/2017.

40. **Mheshimiwa Spika**, mafanikio haya yanatokana na Serikali kuongeza mgao wa fedha katika Sekta ya Afya Nchini kutoka Shilingi **Trillioni 1.988** mwaka 2016/2017 hadi kufika Shilingi **Trillioni 2.222** mwaka 2017/2018. Ongezeko hili ni sawa na **Asilimia 11.77**. Aidha, bajeti ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi imeongezeka kutoka Shilingi **Bilioni 31** mwaka 2015/16 hadi kufikia Shilingi **Bilioni 269** mwaka 2017/18. **Aidha, mafanikio haya pia yametokana na Bohari ya Dawa kuanza kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji badala ya washitiri wa kati waliokuwa wanauzu bidhaa hizo kwa gharama kubwa.**

### Vituo vya kutolea huduma za afya kuwa na vifaa vya kutosha.

41. **Mheshimiwa Spika**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliahidi kuwa, Serikali itahakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya nchini kinakuwa na vifaa vya kutosha ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi.

42. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa ahadi hii ulianza mwezi Aprili 2017, ambapo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilianza kusambaza vitanda ishirini (20) vya kawaida, vitanda vitano (5) vya kujifungulia, magodoro ishirini na tano (25) na mashuka hamsini (50) katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

43. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Agosti 2017; Serikali imekamilisha kusambaza vifaa vifuatavyo: jumla ya vitanda **3,208** katika Halmashauri **162**, magodoro **3,189** katika Halmashauri **160**, mashuka **7,570** katika Halmashauri **159** na jumla ya vitanda **322** vya kujifungulia katika Halmashauri **69** nchini.

44. **Mheshimiwa Spika**, usambazaji wa vifaa hivyo umekamilika kwa asilimia **85**. Serikali inaendelea na zoezi la usambazaji wa vifaa hivyo na kukamilisha kazi hii katika kipindi kifupi iwezekanavyo ili kuwawezesha wananchi kupata huduma bora za afya pindi wanapozihitaji. Jambo la msingi kwa Watendaji katika ngazi mbalimbali ni kuhakikisha katika Vituo vyote vya kutolea huduma za Afya vinavyomilikiwa na Serikali na akina Mama Wajawazito wanapata matibabu bure.

### UWEZESHAJI VIJANA

45. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 Asilimia zaidi ya 35 ya Watanzania ni vijana na hivyo Serikali imeamua kuandaa mpango wa kuwekeza kwao ili nguvu kazi hii iweze kuchangia kikamilifu katika kujenga uchumi wa Taifa kuititia Mpango wa Kutathmini na Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya Mfumo Rasmi wa Mafunzo. Jumla ya vijana **1,000,000** wamelengwa kupata urasimishaji ujuzi kati ya mwaka 2017 na 2021. Hadi sasa vijana kadhaa wanaendelea kunufaika na mpango huu kutoka mikoa mbalimbali.

Miongoni mwa faida za programu hii ni pamoja na kuwasaidia mafundi waliojifunza kuititia sehemu za kazi kupata kazi zenyenye staha na kuwajengea uwezo wa kushiriki na kushindana kikamilifu katika soko la ajira, lakini pia kuinua tija mahali pa kazi na kusaidia waajiri/wenye makampuni kukidhi viwango katika eneo la rasilimali watu. Mpango huu unafadhiliwa kwa asilimia 100 na Serikali na unatekelezwa kwa pamoja na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi – VETA,

### SEKTA YA BARABARA

#### KUANZISHWA KWA WAKALA WA BARABARA ZA VIJJINI NA MIJINI (*Tanzania Rural and Urban Roads Agency-TARURA*)

46. **Mheshimiwa Spika**, Sote tunatambua kilio kikubwa na cha muda mrefu kilichotolewa na Wadau mbalimbali wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwemo Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa na Wananchi na Wadau wa sekta ya barabara kuhusu umuhimu wa kuwa na Wakala wa Barabara Vijiji. Aidha, llani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 katika Ibara ya 39 (a) (iii) (Ukurasa wa 54) inaielekeza Serikali **kuanzisha Wakala/Taasisi itakayosimamia kazi za ujenzi na matengenezo ya barabara za Halmashauri, Miji na Majiji ambazo ziko chini ya TAMISEMI** ifikapo mwaka 2020;

47. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa tayari Serikali imeunda Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini unaojulikana kwa lugha ya kiingereza kama *Tanzania Rural and Urban Roads Agency- TARURA*. Tarehe 2 Julai, 2017 nilipata fursa ya kuuzindua rasmi Wakala huo hapa mjini Dodoma. Wakala huu umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali (Sura 245) na ultangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali Na.211 la tarehe 12 Mei, 2017.

48. **Mheshimiwa Spika**, TARURA imeanzishwa rasmi ikiwa ni jitihada za Serikali za kuimarisha Sekta ya Barabara za Miji na Vijijini. Aidha, Uzinduzi wa Wakala huu ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kuboresha maisha ya wananchi hususan waishio vijijini. Majukumu ya Wakala ni ujenzi, ukarabati na matengenezo ya madaraja na barabara za Vijijini na Mijini zilizokuwa zikitengenezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha usafiri na usafirishaji katika maeneo hayo;

49. **Mheshimiwa Spika**, kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini kunatarajiwa kuondoa kero zifuatazo:

- Barabara za Halmashauri kujengwa chini ya kiwango tena kwa kutumia muda mrefu kuliko makubaliano ya Kimkataba;
- Tabia ya baadhi ya viongozi na watendaji wasio waadilifu wanaozibbia Halmashauri kupitia kandarasi za ujenzi wa barabara; na
- Migongano ya kimaslahi mionganini mwa baadhi ya Madiwani na Watumishi wa Halmashauri katika kusimamia ujenzi wa barabara za Halmashauri kupitia zabuni zinazosimamiwa na Halmashauri

50. **Mheshimiwa Spika**, ni matumaini yangu kuwa TARURA itasaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha mtandao wa Barabara za Vijijini na hivyo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kusafiri na kusafirisha bidhaa za mashambani kwa urahisi ndio kichocheo cha ukuaji wa uchumi vijijini. Naomba kutoa rai kwa Wadau wote wa barabara Nchini wakiwemo Viongozi wa Mamlaka za serikali za Mitaa wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kuusoma Mpango Kazi wa Wakala huo, ili kutoa msukumo katika kuboresha barabara za Vijijini na Mijini zilizopo katika maeneo yao.

51. **Mheshimiwa Spika**, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imepokea hoja ya Waheshimiwa Wabunge ya kupewa ufanuzi wa kutosha kuhusu majukumu ya TARURA. Hoja hiyo itafanyiwa kazi mapema iwezekanavyo ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kusimamia Serikali vizuri kwenye eneo hili la barabara za Halmashauri nchini.

## HITIMISHO

52. **Mheshimiwa Spika**, nimalizie kwa kuwashukuru tena wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Shukrani za pekee ni kwako wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa katuongoza vizuri. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao pamoja na Watumishi wote wa Serikali waliosaidia Serikali kujibu maswali na kuwasilisha Hoja za Serikali hapa Bungeni.

53. **Mheshimiwa Spika**, kipekee namshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha Mkutano huu. Nawashukuru wale wote waliokuwa na jukumu la ulinzi na usalama ili kuhakikisha Mkutano huu unafanya na kumalizika salama. Napenda pia niwashukuru Madereva wote kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa.

Nawashukuru pia Waandishi wa Habari kwa kuhakikisha kuwa Habari za hapa Bungeni zinawafikia Wananchi kwa namna mbalimbali. Mwisho, niwashukuru Wananchi wa Dodoma kwa ukarimu wao wa kutupatia huduma zote muhimu na hivyo kukamilisha Mkutano huu kwa mafanikio makubwa.

54. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi siku ya **Jumanne, tarehe 7 Novemba, 2017** litakapokutana saa 3.00 Asubuhi hapa Mjini Dodoma.

55. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja. (Makofij)

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa Hoja ya Kuahirisha Shughuli za Bunge hadi tarehe aliyoitaja. Wajibu wangu ni kuwahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**SPIKA:** Nichukue nafasi hii nami kutoa shukrani nyingi sana kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wote, Manaibu Mawaziri, kwa jinsi ambavyo mmetupa ushirikiano wa kila aina katika kuhakikisha kwamba, tunafanikisha shughuli za Mkutano huu unaoingia katika historia ya nchi yetu kama Mkutano wa Nane wa Bunge la Kumi na Moja. Waheshimiwa Wabunge kipekee niwashukuruni sana wote kabisa kwa ushirikiano mkubwa sana ambao mmetupatia sisi Meza katika kuhakikisha kwamba, mkutano huu unafikia malengo yake. (Makofij)

Pia, nimshukuru Naibu Spika, kwa kunisaidia sana hapa Mezani, vile vile Wenyeviti wangu, Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Uongozi, tumesaidiana kwa vikao vya kila aina na Kamati zote ambazo mlikuwa na vikao mbalimbali, mliowezesha shughuli hizi kuweza kwenda. Naomba niwashukuruni sana kwa utendaji wa kazi uliotukuka. (Makofij)

Kipekee niwashukuru sana watumishi wa Bunge chini ya Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa sana ambayo mmeifanya usiku na mchana kuhakikisha kwamba, kikao hiki kinaandalialiwa na kinaweza kufanyika hadi kufikia hitimisho lake. Nasema asanteni sana na niwaombe bsi, Watumishi wa Bunge wote kesho Saa tano kamili asubuhi nikutane nanyi kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa tupate kuzungumza kidogo na niweze kuwapongeza watumishi wangu, watumishi wetu. (Makofij)

Niwaombe Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge tuwe pamoja hiyo kesho Saa tano asubuhi, ili tuweze kupata nafasi ya kubadilishana mawazo na Watumishi wetu wa Bunge tuweze kuwasikia na wao waweze kutusikia.

Waheshimiwa Wabunge mionganoni mwetu tuna Wabunge wapya ambaobado hawajapangiwa Kamati, niwataarifu tu kwamba, kazi hiyo tulishaifanya na iko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Kamati yake itakuwa ni Viwanda, Biashara na Mazingira; Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Kamati yake ni Miundombinu; Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, Kamati yake ni Katiba na Sheria; Mheshimiwa Alfredina Apolynary Kahigi, Kamati yake ni Utawala na Serikali za Mitaa; Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Kamati yake ni Huduma na Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, Kamati yake ni Huduma na Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Nishati na Madini; na Mheshimiwa Rehema Juma Migilia, yeye ni Huduma na Maendeleo ya Jamii. (Makofij)

Pia, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba, kuna Sheria ambazo zimesomwa hapa, Miswada ambayo imesomwa hapa kwa Mara ya Kwanza, leo tarehe 15 Septemba. Basi kwa Kanuni ile inayohusika ambayo ni 84(1) inayonipa mamlaka ya ku-allocate Miswada katika Kamati mbalimbali nieleze tu hapa jumla moja kwa moja kwamba, Muswada ule wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania (*The Tanzania Communications Corporation Bill*) wenyewe utaenda Kamati ya Miundombinu.

Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania (*National Shipping Agencies Bill*) wenyewe utaenda Kamati ya Miundombinu pia. Kwa hiyo, Miswada hiyo miwili wa *Telecommunications Corporation Bill* na *Shipping Agencies Bill* itakwenda Kamati ya Miundombinu.

Muswada uliobaki wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No 4 Bill, 2017*) Kamati ya Katiba na Sheria itaanza kuzishughulikia hizo wakati utakapokuwa umekuwa muafaka ili Bunge ijali basi ziweze kupata nafasi ya kufanyiwa kazi mapema.

Ningeomba sana wakati ule wa Kamati tumalize kila kitu kuhusu Miswada hii, isiwe wakati wa kukutana hapa Bungeni ndio tena Kamati zinakimbizana na Miswada. Katika mazingira yawayo yoyote yale tutakapowaita kwa kweli myaangalie mambo haya vizuri mapema na kwa sababu, tunaitana hapahaha Dodoma, basi haina tatizo.

Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wake niwaase tu kuhusu usalama wetu kwamba, tuwe na consciousness ya usalama wa kila mmoja wetu, tusijiachie sana tuwapo katika Majimbo yetu au mahali pengine tunapoenda. Tusikae sana kwenye mabaa mpaka usiku wa manane, yaani tuchukue tu hatua za kuwa makini kidogo na maisha yetu. Kama mnavyosikia matukio ni mengi katika nchi yetu kwa hiyo, ni vizuri, unajua usalama unaanza na wewe mwenyewe kwanza halafu na vyombo vinavyotulinda vinakuwa vinaongezea kidogo. Kwa hiyo, tutazame nyendo zetu, tutazame namna tunavyoishi, wale ambao tumezoea saa nane au saa saba ndio tunarudi nyumbani, basi tuanze kurudi mapema kidogo, na kadhalika.

Vile vile tuangalie usalama wa familia zetu na tuwaambie wapiga kura maana siku hizi watoto wanapotea. Wakiptotea watoto wanauawa kwa hiyo, tuwapelekee ujumbe pia wananchi wetu pia wawe na hiyo consciousness ya usalama kadiri watoto wanavyoenda shule umakini uongezeke, nani anawapeleka shule na nani anaenda kuwachukua shule na mambo yanayofanana na hayo. Kwa hiyo, huo ni ushauri wa ujumla tu.

Mwisho kabisa, Waheshimiwa Wabunge, niwaombee kila la heri, Mwenyezi Mungu awe nanyi muendapo na mtakaporudi. Tukutane tena kama Mwenyezi Mungu atatuweka hai, maana kalenda anayo ye ye menyewe Mwenyezi Mungu.

Hapo ndio mwisho wa matangazo yangu. Katibu!

**DKT. THOMAS D. KASHILILLAH – KATIBU WA BUNGE:**

**WIMBO WA TAIFA**

**SPIKA:** Naomba tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

**SPIKA:** Ahsante sana. Katika kumalizia tukiwa tumesimama, tutakapokwuwa tunaenda nyumbani, basi tuendelee kumwombea mwenzetu Mheshimiwa Lissu kule hospitali, aendelee kupata afya njema kadri Mwenyezi Mungu atakavyomuwezesha na wale wote mtakaopata nafasi ya kumtembelea mpelekeeni salaam.

Wale watu wanaochukua fursa ya kumtembelea mwenzetu na kumuuguza kutuma matusi miongoni mwetu, tuwaombee nao pia na tuwasamehe kwa vile hawajui walitendalo.

Baada ya hapo, Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi tarehe na siku ile iliyotajwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

(Saa 6.03 Mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 7 Novemba, 2017 Saa Tatu Asubuhi)